# MKEMIA NEWSLETTER

ISSN 2714 - 2121 Toleo Namba 005 Julai 2023 - Juni 2024

# WAZIRI MKUU AIPONGEZA MAMLAKA KWA UTOAJI HUDUMA BORA KWA JAMII




18 Allegy-Ugonjwa unaokua kwa kasi duniani

30 Dkt. Jingu ataka wataalam wa tiba asili na tiba mbadala kuwezeshwa



**BW. CHRISTOPHER DEREK KADIO**

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka (GCLA)

Menejimenti na Watumishi wa Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA), tunakupongeza **Bw. Christopher Derek Kadio** kwa kuteuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kuwa **Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali.** Kwa pamoja tunakuahidi kukupa ushirikiano wa kutosha pamoja na Wajumbe wengine wa Bodi katika kipindi chote cha uongozi wako.

# BODI YA UHARIRI




## MWENYEKITI

Dkt. Fidelice Mafumiko

## MHARIRI MKUU

Sylvester Omary

## WAANDISHI

1. Sylvester Omary
2. Judith lema
3. Mwanaheri jazza
4. Okello Thomas
5. Boniphace Majinyali
6. Dkt. Kassim Babu Mapondela

## MSANIFU WA JARIDA

Okello Thomas




## DIRA YETU

Kuwa maabara ya uchunguzi yenye hadhi duniani kwa ajili ya kushughulikia masuala ya Afya, Ustawi wa Jamii na Mazingira.

## DHIMA YETU

Kutoa huduma bora za kimaabara na zenye gharama nafuu na udhibiti kwa serikali, taasisi, asasi na umma kwa ujumla kwa madhumuni ya kulinda afya ya binadamu na mazingira.

14 MAFANIKIO YA MAMLAKA KWA KIPINDI CHA MIAKA MITATU YA MHE. DKT. SAMIA SULUHU HASSAN

Historia ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (Government Chemist Laboratory Authority - GCLA) inaanzia tangu enzi za utawala wa ukoloni wa Mjerumani mwaka 1895.

17 KAMISHNA JENERALI WA DAWA ZA KULEVYA AIPONGEZA GCLA

Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Aretas Lyimo, ameipongeza Mamlaka ya Maabara ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kwa utoaji wa haraka wa ripoti za uchunguzi na uboreshaji wa mifumo ya utendaji kazi.

24 TANZANIA IPO TAYARI KUKABILIANA NA MAAFA YA KIKEMIKALI NA YA KIMIONZI

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa amesema Serikali kwa sasa ipo tayari kuhakikisha usalama wa nchi dhidi ya majanga, maafa na dharura mbalimbali zikiwemo za kikemikali, kibaiolojia, kimionzi na kinyuklia.

# MADINI TEMBO YANAVYOWEZA KULETA ATHARI KWA WATOTO WANAOTUMIA CHUCHU BANDIA

Na Boniphace Majinyali



Matumizi ya chuchu bandia kwa watoto wadogo imeonekana kuwa desturi ya kisasa katika maisha ya jamii kubwa ya watu. Tafiti zinaonyesha kuwa watu wengi hutumia chuchu bandia kama vivutio vya kuwaburudisha watoto (exploratory purposes) au kutumika kama njia ya kuwabembeleza na kuwatuliza watoto wadogo hasa pale wanapokuwa hawajisikii vizuri, mfano wanapoota meno na kupata maumivu. Wengine hutumia chuchu bandia ili kuwafanya watoto kujisikia vizuri na hata kuwafanya kulala usingizi kirahisi.

Matumizi hayo ya chuchu Bandia yanatajwa keleta athari za sumu kutokana na kemikali mbalimbali zinazotumika katika kutengeneza chuchu hizo,na hii hutokea pale ambapo madini tembo ya kadimiamu (Cadmium) na risasi (lead) hufyonzwa kwenye mate ya watoto wanaponyonya chuchu bandia. Hivyo, kupelekea kuwa janga kubwa la afya duniani kote. Kemikali hii aina ya madini tembo hasa Kadimiamu na Risasi yameendelea kusababisha matatizo kama vile magonjwa ya Figo, Moyo, Saratani, Afya ya akili, pamoja na mifumo ya uzazi.

Kote duniani zipo aina mbalimbali za chuchu bandia (nipples); zipo chuchu bandia (nipples) zinazotumika kunyonyesha au kunyonyeshea watoto lakini pia zipo chuchu bandia (pacifiers) ambazo hazitumiki kunywesha watoto badala yake aina hizi za chuchu hutumika kama viburudisho tu kwa watoto wadogo.

Kupitia Makala haya tunaangazia aina hii ya chuchu bandia (pacifiers) ambayo haitumiki kunyonyeshea watoto ispokuwa hutumika kama kiburudisho cha watoto.

Baadhi ya viwanda duniani huzalisha chuchu bandia ambazo hutengenezwa kwa kutumia madini tembo yenye sumu kama vile Kadmiamu na Risasi. Hata hivyo, tafiti zinaonyesha kuwa, madini tembo haya hata yakiwa katika kiwango kidogo yanapoingia mwilini huweza kusababisha athari za kiafya kama zilivyoainishwa hapo juu.

Shirika la Afya Duniani (WHO) liliwahi kueleza kuwa, matumizi ya madini tembo haya katika kiwango chochote hata kiwe kidogo lazima yatakuwa na athari za kiafya kwa watoto wadogo.

***Kwanini madini tembo ya kadmiamu na risasi hutumika kwenye chuchu bandia?***

Viwanda hutumia madini tembo ya Kadmiamu na Risasi kama viimairishi (stabilizing agent), au vilainishi (softening agent) au hutumika kwenye rangi (coloring agent) zinazopakwa kwenye chuchu bandia zinazozalishwa. Madini tembo haya huongezwa kwa makusudi kwa kuwa husaidia uimara wa chuchu bandia ili zisiharibike (autodegradation) zenyewe baadaye kadri zinavyokutana na mazingira tofuati kama vile joto kali au tindikali. Madini tembo haya pamoja na kemikali zingine huwekwa kwenye chuchu bandia kwa viwango tofauti kulingana na utashi wa mzalishaji.

***Kadmiamu na risasi huweza kuvyonzwa kwenye mate wakati mtoto anaponyonya chuchu bandia?***

Kitaalamu kumekuwa na maoni kinzani juu ya uhusiano wa kiwango jumuishi cha madini tembo (total concentration) kwenye chuchu bandia ikilinganishwa na kiasi halisi kinachoweza kuvyonzwa (bioavailable/bioaccessible) kwenye mate kadri mtoto anavyonyonya chuchu bandia kwa muda mrefu.

Hata hivyo, kitaalamu inaaminika kuwa, ni kiasi kile kinachoweza kuvyonzwa na kuingia kwenye mzunguko wa damu mwilini (bioavailable) ndicho kinachoweza kuleta athari za kiafya kuliko kiwango jumuishi cha madini tembo yaliyopo kwenye chuchu bandia. Upatikanaji na uwezo wa madini tembo haya kuleta athari za kiafya mara nyingi hutegemea aina (species) na kiwango (quantities/concentrations) cha madini tembo kinachopatikana kwenye mzunguko wa damu.

Kwa kuwa sayansi na teknolojia vimeendelea kukua, mfumo wa kompyuta uitwao Joint Expert Speciation System (JESS) unaweza kutumika kuigiza mifumo ya mwili wa binadamu (simulation modeling) na kufanya tathmini ya masuala mbalimbali ya kiafya (health risk assessment) ikiwemo kuangalia jinsi gani madini tembo yanavyoweza kuvyonzwa kwenye mfumo huo na kuleta athari kwa binadamu. Kwa kutumia mfumo wa kompyuta (JESS), inathibisha uwezekano mkubwa wa madini tembo ya Kadmiamu na Risasi yanavyoweza kufyonzwa kwenye mate na kisha kuingia kwenye mzunguko wa damu mwilini. Kwa kuweka vitu vyote vinavyounda mate ya binadamu kama vile chumvi, urea, protini na vitu vingine.

Mfumo wa JESS unaweza kuthibitisha kiwango cha madini tembo kinavyoweza kuvyonzwa kwenye mate kwa kiwango cha mpaka asilimia 92 kwa Kadmiamu na asilimia 23 kwa Risasi. Viwango hivi vinaweza kupatikana kwenye kiwango cha pH ya mdomoni inapochukuliwa kuwa kati ya 6.75 na 7.4 na viwango vya madini tembo yanayoowekwa kwenye mate vinaweza chukuliwa kuwa kati ya 1 x 10 -9 na 1 x 10-3 mol/L.

***Maoni na Ushauri***

Kwa kuzingatia kuwa chuchu bandia (pacifiers) zimeendelea kutumika hata katika nchi zinazoendelea, Serikali na wadau wanatakiwa kuchukua tahadhari mapema ili kujiridhisha ubora na usalama wa chuchu bandia zinazoingizwa nchini kwa kubaini viwango vya madini tembo yanayoweza kuwemo kwenye chuchu bandia zinazotumiwa na watoto wadogo katika maisha yao ya kila siku. Vilevile, Jamii inashauriwa kuacha kuendekeza tabia na desturi za kuwapatia watoto chuchu bandia hasa wakati watoto wanapokuwa hawajisikii vizuri au wazazi wanapokuwa katika kutimiza majukumu mengine na hivyo kuamua kutumia chuchu bandia ili kuwabembeleza watoto wadogo na hata kuwafanya kulala usingizi na badala yake sasa wazazi wawanyonyeshe watoto wao. Pia elimu iendelee kutolewa kwa jamii kufahamu juu ya uwezekano wa kemikali zenye sumu kuingia mwilini kupitia watoto wanaponyonya chuchu bandia.

Kutokana na athari hizo, viwanda vinavyozalisha chuchu bandia sasa vijikite katika matumizi ya teknolojia rafiki (green chemistry) isiyokuwa na matokeo yenye athari kwa watumiaji.

# WAJUMBE WA BODI WAKAGUA WADAU WA KEMIKALI

Na Okello Thomas

Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, imewatembelea na kuwakagua zaidi ya wadau 10 wanaohifadhi, kutumia na kusafirisha kemikali kutoka Kanda ya Mashariki.

Akizungumza baada ya ziara hiyo, Mjumbe wa Bodi, Zubeda Salum alisema kuwa imewasaidia kuwafahamu wadau wa Mamlaka katika upande wa utunzaji, usafirishaji na utumiaji wa kemikali hivyo tumeweza kupata mambo mbalimbali ya kushauri na pia kuweza kufanya maamuzi juu ya uzalishaji, utunzaji na usambazaji wa kemikali.

"Kuna wengine wanafanya vizuri sana kwa kufuata sheria za kemikali zikiwemo upangaji mzuri wa mizigo ya kemikali, uimara wa sakafu kwenye maghala lakini kuna wengine tuliwapa ushauri wa papo kwa papo kutokana na mazingira tuliyoyaona hivyo, katika hii ziara tutaweza kufanya maamuzi sahihi kutokana na uelewa tulioupata katika ziara hii," alisema Zubeda.

Kwa upande wake Mjumbe Melchiory Mmbaji, alisema kuwa ziara hiyo ya ukaguzi imewapa nafasi ya kufahamu changamoto mbalimbali zinazowakabili wadau wa kemikali pamoja na wakaguzi wa wadau hao kutoka Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali.

"Baada ya ziara hii, itakuwa rahisi kwa Wajumbe wa Bodi kupitisha maombi ya usajili kwa wadau wa kemikali waliokidhi vigezo na pia ni vyema Menejimenti kuwezesha wakaguzi kutoka Mamlaka ili waweze kufanya kazi kwa ufanisi," alisema Mmbaji.

Naye, Mkurugenzi wa Huduma za Udhibiti, Daniel Ndiyo ameishauri Bodi kuendelea kufanya ziara za kukagua na kufahamu mazingira ya kazi na kuwafahamu wadau wanaowasimamia na wanaokuja kuwapitisha pindi wanapoomba usajili kwani watakapo ona wataweza kufanya maamuzi ambayo yatarejea na mazingira ya wadau wanaotaka usajili.

Mkuu wa Idara ya Masoko na Uhusiano kwa Umma kutoka kampuni ya Jefag, Deogratius Chacha alisema kwamba ujio wa Wajumbe wa Bodi imekuwa furaha na faraja kwao kwasababu wamejifunza mengi kulingana na namna walivyokaguliwa na wanavyofanya kazi kwa hiyo wanategemea kuboresha huduma zao.



*Mkurugenzi wa Huduma za Udhibiti, Daniel Ndiyo (wa tatu kutoka kushoto), akiwaongoza Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka katika kukagua mizigo ya kemikali iliyopo bandari kavu, Dar es Salaam.*



*Wajumbe wa Bodi wakikagua eneo la kuteketeza kemikali iliyopo Mkuranga Mkoani Pwani.*




*Zoezi la upakiaji wa kemikali aina ya Sulphur kwenye makasha kwa ajili ya uhifadhi.*

# WAZIRI MKUU AIPONGEZA MAMLAKA KWA UTOAJI HUDUMA BORA

**Na Mwanaheri Jazza**

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa ameipongeza Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kwa namna inavyoendelea kutoa huduma bora na nzuri kwa jamii.

Waziri Mkuu Majaliwa alitoa pongezi hizo jijini Dodoma wakati alipotembelea banda la Mamlaka katika maonesho ya Wiki ya Madini yaliyofanyika katika ukumbi wa Jakaya Kikwete, jijini Dodoma.

"Sisi hatuna mashaka na Taasisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali, mnafanya kazi nzuri sana ya kuhudumia wananchi, sasa muwahudumie pia na watu wa madini ili kutambua aina ya kemikali zipi nzuri na zipi hazifai kutumika. Kwa hiyo endeleeni kubainisha hayo ili jamii ifanye kazi ya uchimbaji bora" alisema Waziri Mkuu Majaliwa.

Kwa upade wake Katibu Mkuu Wizara ya Madini, Kheri Mahimbali ameishauri Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kufanya kikao cha pamoja na STAMICO na Wizara ya Madini kutengeneza mwongozo utakaosaidia wachimbaji wa madini kujua kiasi cha madini kilichopo ardhini kabla ya kuanza kuchimba.

Kwa upade wake Katibu Mkuu Wizara ya Madini, Kheri Mahimbali ameishauri Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kufanya kikao cha pamoja na STAMICO na Wizara ya Madini kutengeneza mwongozo utakaosaidia wachimbaji wa madini kujua kiasi cha madini kilichopo ardhini kabla ya kuanza kuchimba.

"Sasa mjaribu kukutana mfanye kikao cha pamoja kati yenu, STAMICO na Wizara ya Madini, tengenezeni mwongozo ili uwasaidie wachimbaji wa madini kujua kiasi cha madini kilichopo ardhini kabla hawajaanza kuchimba nadhani hii itakuwa mbinu yenye tija kwa wachimbaji" alisema Mahimbali.

Katika hatua nyingine, wakati akifunga maonesho hayo waziri Mkuu Mh.Kassim Majaliwa ameitaka wizara ya madini kuhakikisha inashirikiana na wadau mbalimbali wa ndani na nje ya nchi ili kupata ufumbuzi wa matumizi ya teknolojia zitakazotumika kuongeza thamani ya madini.

"Sasa nitoe rai kwa wizara ya madini endeleeni kushirikiana na wadau mbalimbali wa ndani na nje ya nchi katika kutatua na kutafuta ufumbuzi wa namna tutakavyotumia teknolojia za uongezaji thamani madini na kuwezesha madini yetu kutumika katika kuzalisha bidhaa mbalimbali, ambazo zinahitajika sana nchini na duniani kote kutokana na kuongezeka kwa mahitaji, pamoja na kuendelea kuongezeka kwa idadi ya watu duniani" alisema Waziri Mkuu Kassim Majaliwa.

Maonesho ya wiki ya madini yalifunguliwa rasmi Juni 20,2024 na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Philip Mpango na kufungwa Juni 27,2024 na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa.



***Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa (kulia) akisoma Jarida la Mamlaka huku akimsikiliza Meneja wa Usajili wa Kemikali na Maabara za Kemia, Musa Kuzumila (kushoto) akieleza majukumu ya Mamlaka kwa wachimbaji wa madini baada ya Waziri Mkuu kutembelea banda la Mamlaka kwenye maonesho ya Wiki ya Madini yaliyofanyika katika viwanja vya Ukumbi wa Jakaya Kikwete, jijini Dodoma Juni 27,2024.***

# MWENYEKITI WA BODI ATEMBELEA WADAU KANDA YA ZIWA

**Na Sylvester Omary**

Mwenyekiti wa Bodi ameupongeza uongozi na wafanyakazi wa Mgodi wa Geita Gold Mining (GGML), kwa kuzingatia Sheria na Kanuni za uhifadhi na matumizi ya kemikali alipotembelea na kukagua mgodi huo uliopo Geita Machi 4, 2024, kwa lengo la kujionea namna mwekezaji huyo anavyozingatia maelekezo ya wataalamu kutoka Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA), juu ya matumizi salama ya kemikali.

Aidha, Mwenyekiti alitembelea bwawa maalumu kwa ajili ya kuhifadhi maji taka yanayotoka kwenye kinu cha kuchenjua dhahabu na kukagua namna ambavyo usanifu wa bwawa hilo umezingatia tahadhari zote ikiwemo kuhakikisha hakuna maji taka yenye mchanganyiko wa kemikali yanatoka nje ya bwawa hivyo hayawezi kuwafikia wananchi na kuathiri afya za binadamu, wanyama na mazingira.

Pia, Profesa Esther Lugwisha amewataka watumishi kutoka taasisi mbalimbali za Serikali waliopo mipakani kufanya kazi kwa ushirikiano na uadilifu ili kujenga taswira nzuri ya Serikali kwa wananchi pamoja na nchi za jirani na pia kutojihusisha na vitendo vya rushwa na kuwa wazalendo kwa nchi yao.

Profesa Lugwisha alitoa wito huo Machi 5, 2024 wakati akizungumza na watumishi wa umma akiwa katika ziara ya kikazi Kanda ya Ziwa katika mpaka wa Tanzania na Uganda (Mutukula), kwa lengo la kuhimiza uwajibikaji na kuzifahamu changamoto zinazowakabili watumishi hao.

"Mtumishi wa Serikali ni taswira ya Serikali katika jamii, hivyo ni wajibu wa kila mtu kuwa na maadili mema yatakayolinda haiba ya Serikali. Kwa hiyo, muwe makini katika utekelezaji wa kazi zenu kwa kuepuka vitendo vya rushwa kwani kwa kufanya hivyo ni sawa na kuisaliti nchi," alisema Profesa Lugwisha.

Kwa upande wake Mkemia Mkuu wa Serikali. Dkt. Fidelice Mafumiko. amewataka watumishi wanaofanya kazi mipakani kuzingatia utunzaji wa siri za Serikali pindi wanapokuwa katika majukumu yao ya kazi kwa kulinda na kuhifadhi vyema nyaraka za Serikali.

Meneja wa GCLA Ofisi ya Kanda ya Ziwa, John Wanjala aliongeza kuwa Mamlaka ipo kuhakikisha kuwa inawafikia wadau wake wote na wananchi kuwapa elimu na pia kudumisha mahusiano mazuri.

Naye, Meneja wa Mazingira kutoka Kampuni ya Uchimbaji dhahabu ya Geita Gold Mining Limited (GGML), Mhando Yusuph alisema wataendelea kufuata Sheria na Kanuni za kemikali na Sera za mazingira ya kampuni na pia kuendeleza ushirikiano na Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA), ili kuhakikisha wanatekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi.



***Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Profesa Esther Lugwisha (katikati), akiwa pamoja na watumishi wa umma kutoka taasisi mbalimbali wanaofanya kazi katika mpaka wa Mutukula Machi 5, 2024. Wa nne kutoka kushoto ni Mkemia Mkuu wa Serikali, Dkt. Fidelice Mafumiko.***

# JAMII YAASWA KUZINGATIA MATUMIZI YA BIDHAA HALISI

**Na Judith Lema**

Kaimu Mkurugenzi wa Jiji la Mwanza, Peter Juma, ameiasa jamii ya watanzania kuzingatia matumizi sahihi ya bidhaa wanazotumia ili kuepuka madhara ya sumu yanayoweza kutokea kwa matumizi holela ya bidhaa hizo.

Kaimu Mkurugenzi aliyasema hayo wakati akifunga mafunzo ya Udhibiti wa Matukio ya Sumu kwa Wahudumu Afya ngazi ya Jamii, Maafisa Mazingira Kata na Wenyeviti wa Serikali za Mitaa wa Halmashauri ya Jiji la Mwanza, Machi 22, 2024.


"Ili tuweza kubaki salama ni muhimu kuacha kufanya mambo kwa mazoea na kuzingatia maelekezo yanayotolewa na wataalamu au kuwekwa kwenye vifungashio za bidhaa tunazotumia ikiwa ni pamoja na uhifadhi salama na matumizi salama wa bidhaa hizo", alisema.

Akitolea mfano wa baadhi ya matukio yaliyotokea jijini Mwanza, ambapo kaya moja iliweza kupoteza watoto watatu waliokufa kwa kula uyoga udhaniwao kuwa na sumu, Peter amesema kuwa mafunzo hayo ni sahihi kwa viongozi hao ambao wapo katika jamii kwa kuwa wamepata uelewa wa kujua visababishi vya sumu na namna ya kuviepuka, hivyo elimu hiyo itawafikia jamii kubwa wanayoishinayo na kwa wakati sahihi.


Kwa upande wake Mkuu wa Kituo cha Taifa cha Kudhibiti Matukio ya Sumu, Yohana Goshashy, alisema kuwa wametoa mafunzo hayo kwa lengo la kulinda jamii ikiwa ni wajibu ambao Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali imepewa kwa Sheria Na. 8 ya mwaka 2016, ambapo Mamlaka kupitia kituo chake cha Taifa cha Kudhibiti Matukio ya Sumu inalo jukumu la kupunguza idadi ya wananchi wanao kufa au kuugua kutokana na sababu mbalimbali za matukio ya sumu.

Ameongeza kuwa Mwaka 2023 kulikuwa na ongezeko la matukio ya sumu na sababu moja wapo ni matumizi yasiyo sahihi ya bidhaa, ikiwemo dawa asili, pombe na dawa tiba zinazotumika hospitalini. Aidha, Mkoa wa Mwanza umeonekana kuwa ni moja ya mikoa iliyokuwa na ongezeko la matukio ya sumu, hivyo Kituo kikaona kuwa ni muhimu kutoa elimu kwa kundi hilo ambalo lipo karibu na jamii na matukio hayo yanatokea katika jamii.

"Ukielimisha jamii hii basi utakuwa umewafikia wananchi wengi kwa kuwa kundi hili linaishi na jamii, hivyo jamii itakuwa imepata elimu na maarifa ya jinsi ya kuepukana na matukio ya sumu, kwa vile matukio haya yanaleta simanzi kubwa kwa jamii na vilevile taifa kupoteza nguvu kazi ya watenda kazi". Alisema Goshashy.



***Mshiriki wa mafunzo akichangia mada wakati wa mafunzo ya udhibiti wa matukio ya sumu kwa Wahudumu Afya ngazi ya Jamii, Maafisa Mazingira Kata na Wenyeviti wa Serikali za Mitaa wa Halmashauri ya Jiji la Mwanza, Machi 22, 2024.***



***"Ukielimisha jamii hii basi utakuwa umewafikia wananchi wengi kwa kuwa kundi hili linaishi na jamii, hivyo jamii itakuwa imepata elimu na maarifa ya jinsi ya kuepukana na matukio ya sumu, kwa vile matukio haya yanaleta simanzi kubwa kwa jamii na vilevile taifa kupoteza nguvu kazi ya watenda kazi".***

**YOHANA GOSHASHY**
Mkuu wa Kituo cha Taifa cha Kudhibiti Matukio ya Sumu

# MAMLAKA YAJIVUNIA MAFANIKIO YA ITHIBATI



***Mkemia Mkuu wa Serikali, Dkt. Fidelice Mafumiko (aliyesimama), akizungumza wakati akifungua kikao kazi cha Wakaguzi wa Ndani wa Mifumo ya Ubora katika ukumbi wa Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania kilichopo Kibaha mkoa wa Pwani.***

**Na Okello Thomas**

Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA), imepata mafanikio katika kupata ithibati ya Maabara zake tano na mbili zilizobaki zitakamilishwa katika mwaka huu wa 2024, kwa kiwango cha kimataifa kwa kiwango cha ISO 17025:2017.

Mkemia Mkuu wa Serikali, Dkt. Fidelice Mafumiko aliyasema hayo wakati akifungua kikao kazi cha Wakaguzi wa Ndani wa Mifumo ya Ubora katika ukumbi wa Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania kilichopo Kibaha mkoani Pwani Aprili 29, 2024.

Dkt. Mafumiko alisema kuwa Mamlaka imeandaa kikao kazi hicho kwa lengo la utekelezaji wa ithibati ya kiwango cha ISO/IEC 17025:2017 na ISO 9001:2015 ambavyo ni mahsusi katika kuongeza umahiri katika utendaji wa kila siku katika maabara, kuimarisha hadhi ya Maabara za Mamlaka kulingana na viwango na matakwa ya kimataifa pamoja na kuiwezesha Mamlaka kuongeza wigo wa ithibati katika maabara zake.

"Wakaguzi wa ndani ni mhimili muhimu sana ili kuhakikisha kuwa mifumo yetu inakwenda kama inavyotakiwa, hivyo ni muhimu kwa kila mkaguzi kutambua dhamana aliyokabidhiwa kwa ajili ya kutimiza matakwa ya ithibati na kuimarisha utendaji kazi wa Maabara unaozingatia viwango vya kimataifa," alisema Dkt. Mafumiko.

Aidha, Dkt. Mafumiko amewataka wakaguzi wa ndani kuongeza juhudi kwa kujituma katika kutekeleza, kusimamia na kukagua mifumo ya ubora kulingana na matakwa ya mifumo bora ya maabara ili kulinda ithibati na kuitekeleza kwa vitendo na kuleta sifa nzuri kwa Mamlaka na Taifa kwa ujumla.

Kwa upande wake Mkuu wa Kitengo cha Udhibiti Ubora na Usimamizi wa Vihatarishi Benny Mallya, alisema wakaguzi wa ndani wa mifumo wataendelea kutekeleza majukumu ya ukaguzi kwa umahiri na pia kuhakikisha Mamlaka inatetea na kusimamia vyema ithibati za maabara zilizopatikana.



***Mkemia Mkuu wa Serikali, Dkt. Fidelice Mafumiko (katikati), akiwa pamoja na Wakaguzi wa Ndani baada ya kufungua kikao kazi cha Wakaguzi wa Ndani wa Mifumo ya Ubora katika ukumbi wa Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania kilichopo Kibaha mkoa wa Pwani.***

# MHIJE: KUTOKA KIDATO CHA NNE MPAKA KUWA MKUU WA HUDUMA ZA UFUNDI GCLA

**Judith Lema na Mwanaheri Jazza**

Agosti 14 mwaka1945 katika kijiji cha Malangali, Wilaya ya Ludewa katika Mkoa wa Njombe ilipatikana neema ya mtoto wa kiume katika nyumba ya mzee Joshua Mhije na Bibi Maria Msigwa ambao waliamua kumpatia jina la Zabron.

Ama kwa hakika Mzee Joshua Mhije na Bibi Maria Msigwa hawakuweza kutambua kama neema ya ujio wa kijana huyo ingeacha alama ya kusisimua ya kuitumikia Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kwa takribani miaka 19 katika Kitengo cha huduma za mitambo yaani (Technical Services), ambapo kulifanyika mapinduzi makubwa ya mitambo kutoka Analogia kwenda Digitali hali iliyorahisisha utendaji kazi na kuongeza ufanisi na wateja katika Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali.

Katika Makala hii tutaangazia historia ya Mzee Zabron Joshua Mhije, kuanzia elimu yake hadi utumishi wake katika Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali ikiwemo Mafanikio, Mchango wake kwa Mamlaka na taifa kwa ujumla pamoja na changamoto alizopitia katika utumishi wake.

***Safari ya Elimu***

Mzee Zabron Joshua Mhije alianza shule ya msingi mnamo mwaka 1952 katika shule ya msingi Malangali, ambapo alisoma mpaka darasa la nne na ilipofika mwaka 1955 alihamia shule ya msingi Kongwa iliyopo mkoani Dodoma kwa kuwa baba yake alihamishiwa kikazi mkoani humo.

Mwaka 1958 alifanikiwa kufaulu na kwenda "middle School" katika shule iliyojulikana kwa jina la Mototo ambapo alihitimu mwaka 1961.

Baada ya hapo alifanikiwa kujiunga na kidato cha kwanza katika Shule ya Sekondari Mpwapwa mkoani Dodoma mwaka 1962, ambapo alisoma kidato cha kwanza hadi cha nne na kuhitimu mwaka 1965.

***Safari ya Ajira***

"Mwaka 1966 nilijiunga rasmi katika Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali ambapo kipindi hicho ilikuwa ni sehemu ya idara katika Wizara ya Afya na ilinilazimu kuanza kazi kwa kujitolea yaani (Internship) na nilipangiwa kwenye sehemu ya Routine Section ambayo ilikuwa inafanya uchunguzi wa maji na vyakula. Kwa kipindi hicho ilikuwa unapangiwa kufanya kazi katika kitengo kwa muda wa miaka miwili kisha unapelekwa kitengo kingine mpaka ufahamu kazi zote zinazofanyika katika vitengo vyote vya maabara.

Baada ya hapo nikawa nahamia vitengo mbalimbali ambapo nilienda kitengo cha sayansi jinai, nikaenda kitengo cha chakula na baadae nikaenda maabara ya DNA, ambapo kipindi hicho Mkemia Mkuu wa Serikali alikuwa Khomo, ambaye alitokea Afrika ya Kusini.

Katika kipindi chote hicho mazingira ya kazi yalikuwa ni mazuri na tulikuwa tukipewa mafunzo ya kazi mara kwa mara ambayo yalituwezesha kufanya vizuri kazi zetu" alisema Mzee Zabron.

Kwa mujibu wa Mzee Zabron anasema katika vitengo vyote alivyopangwa yeye, alidumu zaidi katika kitengo cha huduma za mitambo (Technical Services) na alifurahia sana kufanya kazi katika kitengo hicho.

"Wakati ninaanza kazi kulikuwa na kitengo cha lishe, chakula, dawa, jinai na hiki cha huduma za mitambo, mimi nilidumu kitengo cha mitambo na nilipenda mazingira ya kazi yalikuwa mazuri na ndio nilikuwa mkuu wa kitengo hicho na kilikuwa kinashughulika na uchunguzi wote wa kimaabara na mimi nilikuwa nathibitisha yaani kutoa majibu baada ya uchunguzi, na hapa pia ndipo palinipatia nafasi ya kwenda Chuo Kikuu cha MSALA kujifunza zaidi masuala ya mitambo." alisema Mzee Zabron.

***Changamoto alizopitia***

"Kwa kweli changamoto ilikuwa kwenye kitengo cha uchunguzi wa jinai kwa sababu ilikuwa unakwenda moja kwa moja mahakamani kutoa ushahidi na kesi nyingi zilikuwa nzito mno kwa hiyo ilikuwa ni kitengo kinachonipa hofu"

Mzee Zabron anawashauri vijana waliopo sasa kwenye utumishi wa umma kwamba wafanye kazi kwa bidii, uaminifu na weledi mkubwa, waachane na tamaa ya pesa na mali.
Pia alitoa ushauri kwa uongozi wa Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kuendelea kuwajengea uwezo vijana ili waendane na wakati uliopo wa sayansi na teknolojia katika utendaji kazi.

Mzee Zabron kwa sasa ni mstaafu, anakula pensheni yake baada ya kulitumikia Taifa na kustaafu utumishi wa umma takribani miaka 19 iliyopita. Katika maisha yake binafsi Mzee Zabron alimuoa Bi.Joyce Mageyekwa na kujaaliwa kupata watoto watatu ambao anaishi nao mpaka sasa.



**MZEE ZABRON JOSHUA MHIJE**
Mtumishi Mstaafu wa GCLA

# WATUMISHI WAPYA WAPEWA MAFUNZO YA AWALI

**Na Mwanaheri Jazza**

Waajiriwa Wapya na Watumishi waliohamia katika Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, wapewa mafunzo ya awali (Induction) kazini kwa lengo la kuwakaribisha rasmi kujiunga na Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA), pamoja na kuwasaidia kupata uelewa wa Sheria, Taratibu, Kanuni na Misingi ya Utumishi ili kutimiza malengo ya Serikali.

Mafunzo hayo yalltolewa kwa watumishi wapya 25, Disemba 11, 2023 katika ukumbi wa Bunge jijini Dar es Salaam ambapo mada mbalimbali ziliweza kuwasilishwa na viongozi kutoka Mamlaka zikiwemo majukumu ya Kurugenzi zilizopo, Sheria, Kanuni na Taratibu katika Utumishi wa Umma pamoja na kufahamu umuhimu wa huduma kwa wateja, mawasiliano ya kiofisi na matumizi ya mitandao ya kijamii.

Mkemia Mkuu wa Serikali, Dkt. Fidelice Mafumiko alisema Mamlaka imeweka utaratibu wa kutoa mafunzo ya awali kwa Watumishi wote wanaojiunga na Mamlaka kwa njia ya ajira mpya au uhamisho kwa lengo la kuwafahamisha majukumu na utamaduni wa taasisi, hivyo, amewataka watumishi wapya kuwa watiifu kwa kufanya kazi kwa kuheshimu kanuni za Utumishi wa umma na weledi ili kuendelea kujenga taswira nzuri ya taasisi.

"Mamlaka inatoa mafunzo haya kwa lengo la kuhakikisha Watumishi wote wa Mamlaka wanaelewa vema majukumu ya Mamlaka na utamaduni wake, hivyo kuwezesha utekelezaji wa majukumu wenye ufanisi zaidi kwa kuwa taasisi hii ni miongoni mwa taasisi muhimu za Umma ambayo inahitaji watumishi wenye uadilifu wa hali ya juu," alisema Dkt. Mafumiko.

Aidha, Mkemia Mkuu wa Serikali aliongeza kuwa mafunzo hayo yatawawezesha kujua vyema Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, kwa maana ya majukumu yake ya msingi kwa Serikali na Jamii ya Watanzania na kujifunza umuhimu wa utunzaji wa siri ambao ni moyo wa utendaji wa Mamlaka.

Dkt. Mafumiko aliwasihi washiriki hao wa mafunzo kuwa wasikivu katika kipindi chote cha mafunzo na pia wasisite kuuliza maswali pale inapolazimu ili waweze kutoka wakiwa wameelewa namna shughuli zinavyofanyika katika taasisi na namna ya kuenenda katika kipindi chote watakapokuwa watumishi wa Mamlaka.



***Mkuu wa Kitengo cha Huduma za Sheria, Gilbert Ndeoruo (aliyesimama) akiwasilisha mada kuhusu majukumu ya Kitengo cha Sheria kwa waajiriwa wapya na watumishi waliohamia Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali.***



***Mtumishi mpya wa Mamlaka, Lukito Lutego (kushoto), akiuliza swali wakati wa mafunzo elekezi kwa waajiriwa wapya na watumishi waliohamia Mamlaka.***

***"Mamlaka inatoa mafunzo haya kwa lengo la kuhakikisha Watumishi wote wa Mamlaka wanaelewa vema majukumu ya Mamlaka na utamaduni wake, hivyo kuwezesha utekelezaji wa majukumu wenye ufanisi zaidi kwa kuwa taasisi hii ni miongoni mwa taasisi muhimu za Umma ambayo inahitaji watumishi wenye uadilifu wa hali ya juu,"***

***Dkt. Mafumiko - Mkemia Mkuu wa Serikali***

# WATUMISHI WA MAMLAKA WATAKIWA KUIMARISHA MISINGI YA UTOAJI HUDUMA



***Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano kwa Umma, Sylvester Omary (aliyesimama) akiwasilisha mada kuhusu utoaji wa huduma bora kwa wateja kwenye Mafunzo ya Huduma kwa Wateja yaliyotolewa kwa watumishi wa Mamlaka waliopo Makao Makuu Dodoma. Mafunzo hayo yalifanyika katika ukumbi wa Mamlaka jijini Dodoma Novemba 16, 2023.***

**Na Okello Thomas**

Mkemia Mkuu wa Serikali, Dkt. Fidelice Mafumiko amewataka watumishi wa Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kuendelea kutoa huduma bora zaidi kwa wateja wanaowahudumia.

Akizungumza wakati akifungua Mafunzo ya siku moja ya Huduma kwa Mteja yaliyofanyika katika ukumbi wa Mamlaka jijini Dodoma Novemba 10, 2023. Mkemia Mkuu wa Serikali alisema kuwa Mafunzo hayo ni muhimu kwa kuwa yanasaidia kuimarisha utoaji huduma kwa wateja.

"Tutambue jukumu letu la msingi na kila mmoja kwenye taasisi aelewe kwamba ana wajibu wakufahamu majukumu ya Mamlaka, huduma na maeneo anayofanyia kazi ili mteja anapokuja awe na uwezo wa kumuelekeza, kumuhudumia lakini na kutambua kwamba tunahitaji kutokuwa na urasimu, kutoa huduma zilizo bora na uwajibikaji wa pamoja," alisema Dkt. Mafumiko.

Aidha, Mkemia Mkuu wa Serikali aliongeza kuwa, kutoa huduma bora kutaongeza ubunifu lakini pia kubadilika kimtazamo kwasababu Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali haisimami yenyewe bali ni taasisi mtambuka hivyo ni vyema kuongeza tija zaidi.

Naye, mwezeshaji wa mafunzo ambaye ni Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano kwa Umma, Sylvester Omary alisema utoaji wa huduma bora kwa mteja ni njia mojawapo ya kujitangaza hivyo ni muhimu kwa kila mtumishi kufanya jitihada za kubadili mtazamo na kuwa na mtazamo chanya ili kuweza kuwahudumia wateja kwa namna bora zaidi. Pia, amewaasa watumishi kufanya kazi kwa mshikamano na upendo ili kuweza kujenga mahusiano mazuri baina ya watumishi wenyewe na watumishi kwa wateja.

Kwa upande wake Mkemia Zabibu Duru, ameahidi kuzingatia mafunzo hayo kwa kuendelea kuwakilisha vyema Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali katika utoaji huduma bora kwa mteja na kuhakikisha mteja anaridhika na huduma za Mamlaka.

"Tumefarijika baada ya kupata elimu hii ya huduma kwa mteja maana imetujenga na kwa muktadha huo, ili kujenga na kulinda jina la taasisi tunapaswa kuendelea kutoa huduma bora kwa wateja wetu," alisema Zabibu.

# WATANZANIA WAHAMASISHWA KUFANYA MAZOEZI

**Na Mwanaheri Jazza**

Watanzania kote nchini wameshauriwa kutenga muda wa kufanya mazoezi ili kuepukana na magonjwa yasiyoambukiza ambayo yamekuwa yakiongezeka kila siku.

Akizungumza jijini Dar es Salaam wakati wa ufunguzi rasmi wa ufanyaji mazoezi uliiongozwa na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa katika ufukwe wa Coco beach, Mkemia Mkuu wa Serikali, Dkt. Fidelice Mfumiko amesema utaratibu wa ufanya wa mazoezi hayo utasaidia kulinda afya za wananchi wasipatwe na magonjwa ya kuambukiza.

"Mimi naunga mkono sana uamuzi wa serikali kupitia Mhe. Waziri Mkuu Kassim Majaliwa lakini na wito wa Waziri wetu wa Afya, Ummy Mwalimu kwamba tujitokeze kwenye mazoezi haya kama ambavyo yameanzishwa leo katika jiji la Dar es Salaam, Mimi kwa nafasi yangu kama Mkemia Mkuu wa Serikali nasema mazoezi haya yatasaidia sana kulinda afya za wananchi kwa sababu yatatukinga tusipate magonjwa yasiyoambukiza yanayosumbua sana wananchi kama ambavyo yameainishwa,ugonjwa wa kisukari pamoja na shinikizo la juu la damu". alisema Dkt. Mafumiko.

Dkt Mafumiko pia amewataka watumishi wa Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kuendeleza utaratibu wa kufanya mazoezi mara wanapomaliza majukumu yao ya kazi ili kulinda afya zao pamoja na kujenga nguvu kazi yanye afya kwa taifa.

"Niendelee kuwakumbusha watumishi wenzangu wa Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali,kama ambavyo sisi tumetoa fursa kwa kufanya mazoezi ofisini, kwa Kanda ya Dodoma na Dar es Salaam tuna gym, basi tuwe tunafanya mazoezi ili tujenge nguvu kazi yenye afya ya mwili, roho na akili", alisema Dkt Mafumiko.

Kwa upande wake Kaimu Mkurugenzi wa Uchunguzi wa Bidhaa na Mazingira, Dkt Shimo Peter, amesisitiza ufanyaji wa mazoezi wenye kuzingatia mtindo bora wa maisha kwa kula vyakula vyenye afya na kujenga mwili.

"Naishukuru serikali kwa kuruhusu utaratibu huu na kuhamasisha watanzania, lakini pia namshukuru Mkemia Mkuu wa Serikali kwa kutenga bajeti ya kufanya mazoezi kila siku. Lakini pia niwashukuru wafanyakazi wenzangu ambao wamekuwa wakifanya mazoezi kila siku kwani tunafahamu mazoezi ni afya ila kitu cha muhimu na kuzingatia ni kwamba ni chakula gani unakula ambacho kinaendana na mazoezi unayofanya, kwa hiyo ukila chakula ambacho ni safi na salama ambacho hakiwezi kujitenga kwenye mwili kitakufanya uweze kuwa na afya njema ambayo itakuwezesha kutenda kazi zako za kila siku bila kupata magonjwa yeyote ya kuambukiza", alisema Dkt. Shimo.

Nae Mkemia kutoka Ofisi ya Kanda ya Mashariki, Omary Edward amesema fursa hiyo iliyotolewa na serikali itawanufaisha watumishi kuiwezesha miili yao kuwa imara na kufanya kazi kwa bidii.

"Mimi kama mtumishi pamoja na watumishi wengine utaratibu huu wa ufanyaji mazoezi utatunufaisha kwa kuwezesha miili yetu kuwa imara na kuwa na nguvu ya kufanya kazi", alisema Edward.

Serikali imetangaza rasmi kuwa kuanzia jumamosi ya tarehe 04 Mei,2024 na jumamosi zote zinazofuata kuwa ni siku ya kufanya mazoezi kwa mikoa yote ya Tanzania ili kupunguza kasi ya ongezeko la magonjwa yasiyoambukiza.




***Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa (katikati), akiongoza viongozi na wanamichezo katika mazoezi na matembezi ya kilomita 10 yaliyoanzia Coco Beach hadi mzunguko wa Hospitali ya Agha Khan na kurudi Coco Beach kwa lengo la kuhamasisha ufanyaji wa mazoezi ili kujikinga na magonjwa yasiyoambukiza Mei 4, 2024.***

# MAFANIKIO YA MAMLAKA KWA KIPINDI CHA MIAKA 3 YA DKT. SAMIA

Historia ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (Government Chemist Laboratory Authority - GCLA) inaanzia tangu enzi za utawala wa ukoloni wa Mjerumani mwaka 1895. Enzi hizo Maabara ilikuwa na jukumu la kufanya utafiti wa magonjwa ya ukanda wa joto (Tropical diseases) hususani Malaria na Kifua Kikuu. Baada ya Uhuru, Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali ilikuwa mojawapo ya Idara chini ya Wizara ya Afya hadi Mwaka 1999 ilipopandishwa hadhi na kuwa Wakala chini ya Sheria ya Wakala za Serikali, Sheria Na. 30 ya Mwaka 1997. Aidha, Mwaka 2016, Wakala ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali ilipandishwa hadhi tena na kuwa Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali chini ya Sheria ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Sheria Na. 8 ya mwaka 2016.

***Uwekezaji kwenye Miundombinu ya Uchunguzi wa Kimaabara***

Katika kipindi cha Miaka mitatu ya Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Uongozi wa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali imeweza kujenga jengo la Makao Makuu ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, eneo la Medeli jijini Dodoma lenye Thamani ya **Shilingi Bilioni 8.14.**



***Jengo la Makao Makuu ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali lililopo eneo la Medeli Jijini - Dodoma***

Aidha, Mamlaka ipo katika hatua za awali za Ujenzi wa majengo ya Ofisi na Maabara katika Ofisi za Kanda ya Kusini iliyopo Mtwara, Kanda ya Ziwa Jijini Mwanza na Kanda ya Mashariki jijini Dar es Es Salaam unaokadiriwa kugharimu kiasi cha jumla ya Shilingi Bilioni 5. Miradi hii ikikamilika itaboresha mazingira ya kufanyia kazi na utoaji huduma kwa wananchi wa mikoa ya Dar es Salaam na Pwani, mikoa ya Kanda ya Ziwa na mikoa ya Kanda ya Kusini.

***Uwekezaji kwenye Mitambo na vifaa vya Kisasa vya Uchunguzi wa Kimabaara***

Katika kipindi cha miaka mitatu ya Serikali ya Awamu ya Sita Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali imeweza kununua mitambo na vifaa vya kisasa kwa ajili ya kuendelea kuboresha huduma za uchunguzi wa kisayansi wa kimaabara vyenye thamani ya Shilingi Bilioni 14. Mitambo na vifaa hivi ni pamoja na mitambo mikubwa Kumi na mbili (12) na midogo 205.

Mitambo hii ni kwa ajili ya kuimarisha uchunguzi wa kimaabara na kuendelea kutoa huduma bora za uchunguzi wa Kisayansi wa kimaabara kwa wananchi kwa haraka na kwa wakati.



***Mtambo wa kisasa wa LCMS MSMS (Obtrap Exploris – 240) uliopo katika Maabara ya Dodoma unavyoweza kufanya uchunguzi wa dawa za kulevya na sampuli nyingine kwa haraka***

***Uwekezaji katika Mafunzo kwa Wataalam***

Katika kipindi cha Miaka mitatu ya Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Uongozi wa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali imewezesha watalaam 28 kuhudhuria mafunzo ya muda mrefu. Aidha, watumishi 147 walihudhuria mafunzo ya muda mfupi ndani na nje ya nchi; Watumishi 56 waliwezeshwa kuhudhuria mikutano ya kitaaluma (Professional Bodies), na watumishi 23 waliwezeshwa kupata mafunzo ya awali ya Utumishi wa Umma baada ya kuajiriwa.

Mafunzo haya yameweza kuwajengea uwezo watumishi wa Mamlaka katika kutekeleza majukumu yao kwa weledi na ufanisi mkubwa. Pia, mafunzo hayo yamewezesha Mamlaka kuongeza ubora wa utoaji huduma kwa wananchi.

***Ufanisi wa Huduma za Uchunguzi wa Kimaabara***

***Uchunguzi wa kimaabara***

Uwekezaji wa miundombinu wezeshi ya uchunguzi wa Maabara umeongeza ufanisi wa uchunguzi ambapo mwaka 2021 wastani wa sampuli/vielelezo 155,817, sawa na asilimia 139.94 ya lengo la wastani wa kuchunguza sampuli/vielelezo 111,349 ulifanyika. Aidha, katika mwaka 2022, sampuli 212,306 sawa na asilimia 133.9 ya lengo la kuchunguza sampuli 158,600 zilifanyiwa uchunguzi wa kimabaara. Vilevile, Katika kipindi cha Julai hadi Disemba 2023, sampuli 84,352 zilifanyiwa uchunguzi sawa na asilimia 87.45 ya lengo la kuchunguza sampuli 96,450. Matokeo ya uchunguzi huu yanasaidia Mamlaka ombezi na vyombo vya maamuzi kisheria kufanya maamuzi stahiki na kwa wakati.

***Mchango wa utoaji wa matokeo ya Uchunguzi wa Sampuli kwa wakati***

Uchunguzi wa Kisayansi wa sampuli na utoaji matokeo kwa wakati unasadia kuleta **haki, amani na utulivu** wa nchi kwa kutoa ushahidi wa kitalaam Mahakamani kwenye yanayotokana na uchunguzi wa sampuli na vielelezo mbalimbali vya masuala ya jinai. Vile vile, uchunguzi huo huwezesha kuzikwa kwa **miili ya Wahanga** wa majanga mbalimbali kwa kuzingatia dini, mila na desturi za wahusika pamoja na kutatua migogoro kwenye jamii (**uhalali wa wazazi kwa mtoto, mirathi**). Uchunguzi wa kisayansi wa kimaabara una mchango pia kwa **wagonjwa** wanaotakiwa kupandikizwa figo na utambuzi wa jinsi tawala kwa ushirikiano na Madaktari Bingwa. Mchango mwingine wa uchunguzi wa kimaabara ni pamoja na kutambua aina ya sumu kwa wagonjwa wanaodhaniwa kuvuta, kula au kunywa chakula chenye sumu ili kupata tiba sahihi na kwa wakati na kuokoa maisha. Uchunguzi wa kimaabara unasaidia pia kuhakiki ubora na Usalama wa bidhaa za Viwandani na Kilimo kwa ajili ya kulinda afya ya Jamii na mazingira.



***Wataalam wakisoma matokeo ya kiuchunguzi wa kimaabara kwa ajili ya kuandaa ripoti.***

***Usimamizi wa Kemikali ili Kulinda Afya ya Binadamu na Mazingira***

Mamlaka inatekeleza jukumu la usimamizi na udhibiti wa kemikali kupitia utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Kemikali za Viwandani na Majumbani, Sheria Na. 3. ya Mwaka 2003. Aidha, utekelezaji wa Sheria hiyo unafanyika kupitia Usajili wa wadau, ukaguzi wa maghala na maeneo ambapo kemikali zinatumika na Utoaji vibali vya kuingiza au kusafirisha kemikali.




***Zoezi la ukaguzi wa uhifadhi wa kemikali hatarishi.***

***Usimamizi wa Kemikali ili Kulinda Afya ya Binadamu na Mazingira***

Mamlaka inatekeleza jukumu la usimamizi na udhibiti wa kemikali kupitia utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Kemikali za Viwandani na Majumbani, Sheria Na. 3. ya Mwaka 2003. Aidha, utekelezaji wa Sheria hiyo unafanyika kupitia Usajili wa wadau, ukaguzi wa maghala na maeneo ambapo kemikali zinatumika na Utoaji vibali vya kuingiza au kusafirisha kemikali.

***a) Usajili wa Wadau***

Mamlaka imeendelea kufanya maboresho ya kuharakisha mchakato wa usajili wa kampuni zinazojihusisha na biashara ya kemikali. Katika kipindi cha miaka mitatu ya Serikali ya Awamu ya Sita kumekuwa na ukuaji wa biashara kwa wadau wanaojihusisha na biashara ya kemikali, ambapo wadau wameongezeka kutoka Wadau 2,125 Mwaka 2021 hadi Wadau 4,181 kufikia Disemba, 2023 sawa na ongezeko la asilimia 97 la wadau waliosajiliwa.

***b) Ukaguzi wa Maghala***

Katika kuhakikisha kuwa kemikali zinatumika kwa usalama na kwa kufuata taratibu zote zinazohitajika ili kulinda afya za binadamu na mazingira, na pia ili kuhakikisha kuwa kemikali zinazoingizwa nchini ni zile ambazo zinaruhusiwa kuingia, Mamlaka hufanya ukaguzi wa mara kwa mara kwenye maghala yanayohifadhi kemikali na maeneo ya mipaka. Hivyo katika kipindi cha miaka mitatu (3), Mamlaka imefanya ukaguzi wa maghala 5,335 ya kuhifadhia kemikali sawa na asilimia 118.6 ya lengo la kukagua maghala 4,500.

***c)*** Utoaji wa Vibali vya Kuingiza au Kusafirisha Kemikali

Mamlaka imeweza kudhibiti uingizaji na usafirishaji wa kemikali hatarishi na zile zinazodhibitiwa chini ya mikataba ya kimataifa ili kulinda afya ya binadamu na mazingira kwa kutoa vibali vya kuingiza na kusafirisha kemikali hizo. Katika kipindi cha miaka mitatu (3), kumekuwa na ongezeko la vibali vya uingizaji wa kemikali kutoka 40,270 kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 hadi 101,057 kufikia Disemba, 2023 sawa na ongezeko la asilimia 151 ya vibali vilivyotolewa. Sababu ambayo imepelekea kuongezeka kwa vibali ni kuwepo kwa mazingira mazuri ya biashara na uwekezaji yaliyowekwa na Serikali ya Awamu ya Sita.

***d) Kuboresha Mazingira ya Biashara na Kukua kwa Biashara ya Kemikali***

Katika kipindi cha miaka mitatu (3) cha uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita, Mamlaka imendelea kuboresha mazingira ya biashara ya kemikali nchini hasa zile za kimkakati zinazotumika kwenye uchimbaji na uchenjuaji wa madini hapa nchini na nchi za Zambia na Congo. Ambapo:

i. Kemikali ya Ammonium Nitrate ambayo hutumika hasa katika ulipuaji wa miamba wakati wa uchimbaji madini nchini na nchi za Zambia na DR. Congo imeongezeka kutoka Tani **135,445** Mwaka Fedha 2021/2022 hadi Tani **319,889.5** kufikia Disemba, 2023 sawa na ongezeko la asilimia 136.18.

ii. Kemikali ya Salfa ambayo hutumika hasa katika mchakato wa uchimbaji na uchenjuaji wa madini ya shaba nchi za Zambia na DR. Congo kupitia bandari ya Dar es Salaam imeongezeka kutoka Tani **396,982** Mwaka Fedha 2021/2022 hadi Tani **1,132,644** kufikia Disemba 2023, sawa na ongezeko la asilimia 185.31.

hadi Tani **1,132,644** kufikia Disemba, 2023 sawa na ongezeko la asilimia 185.31.

iii. Kemikali ya Sodium Cyanide ambayo hutumika katika uchenjuaji wa madini ya dhahabu nchini na nchi za Zambia na DR. Congo kupitia bandari ya Dar es Salaam zimeongezeka kutoka Tani **41,461** Mwaka Fedha 2021/2022 na Tani **37,331** kufikia Disemba, 2023 sawa na ongezeko la asilimia 156.47 Sababu ambazo zimepelekea kuongezeka kwa uingizaji wa kemikali hizo kupitia Bandari ya Dar es Salaam ni kuwepo kwa maboresho ya miundombinu ya bandari na mahusiano mazuri kati ya Nchi yetu na nchi Jirani yaliyowekwa na Serikali ya Awamu ya Sita. Vile vile, kupitia elimu kwa umma/wadau wa biashara ya kemikali kumekuwa na ongezeko kubwa la wadau wanaotimiza matakwa ya sheria za nchi ikiwemo sheria ya usimamizi na udhibiti wa kemikali.

**3.1 Huduma za Mamlaka kupitia Matumizi ya TEHAMA**

Mamlaka imeendelea kutengeneza/kujenga na kusimika mifumo mbalimbali ya TEHAMA kupitia watalaam wake wa ndani. Mifumo hii imeimarisha na kuongeza matumizi ya TEHAMA ndani ya Mamlaka.

**a)** Mfumo wa Usajili na Utoaji Vibali kwa Wadau wa Kemikali (Customer Chemicals Management Portal - CCMP); (Kutoka siku saba hadi muda wa saa moja).

**b)** Mfumo wa Kuratibu taarifa za Maabara (Laboratory Management Information System) (kuunganisha Mfumo wa Haki Jinai ili kubadilishana taarifa za matokeo ya uchunguzi wa Maabara na mifumo mingine ya Haki Jinai).

**c)** Mfumo wa kutoa ushahidi kwa ki-electroniki (Video conferencing and Virtual courts) – (Kupunguza gharama kwa serikali kwa wataalam kusafiri kwenda kutoa ushahidi mahakamani kwenye mnyororo wa Haki Jinai).

**d)** Mfumo wa Usimamizi wa taarifa za watoa ushahidi mahakani (Expert Witness Management System) – kuwezesha ofisi ya Taifa ya Mashtaka na Mahakama kupata taarifa za mwendendo watoa ushahidi.

Ujenzi na Usimikaji wa mifumo hii umetumia wataalamu wa ndani wa Mamlaka kwa kushirikiana na wataalam wa Serikali Mtandao.

**Huduma za Kimaabara kwa Viwango vya Ubora wa Kimataifa**

Mamlaka imefanikiwa kuendelea kutoa huduma za Uchunguzi wa Kimaabara kwa Viwango vya Ubora vya Kimataifa. Viwango hivyo vya ubora vinatambulika kwa kupata Ithibati. Ithibati ya umahiri wa maabara ni moja ya mafanikio makubwa sana kwa Mamlaka na kwa Tanzania kwa ujumla, ambapo Mamlaka inakuwa na uwezo wa kupokea na kufanya uchunguzi wa sampuli kutoka ndani na nje ya nchi na kutoa matokeo yanayokubalika duniani.

Mamlaka inatekeleza mifumo miwili ya ubora na umahiri ya kimataifa, ambayo ni Ithibati ya Mifumo ya Ubora (ISO 9001:2015) iliyohuishwa kwa mara tatu mfululizo – Mifumo ya Ubora ya uendeshaji wa Mamlaka umekubalika Kimataifa na Ithibati katika Umahiri wa uchunguzi wa kimaabara (ISO 17025:2027) katika maabara zake nne – Matokeo ya Uchunguzi wa Kimaabara yanakubarika Kimataifa.



***Mtaalam wa Maabara, Brina Kiwia akifanya uchunguzi wa sampuli kwa kutumia mtambo wa Gas Chromatography Mass Spectrometer (GC - MS/MS).***



***Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, akimsikiliza Mkemia Mkuu wa Serikali, Dkt. Fidelice Mafumiko, akielezea kazi za uchunguzi wa kimaabara zinazofanywa na Mamlaka ikiwemo uchunguzi wa kimaabara wa vielelezo mbalimbali vya dawa za kulevya zinazowasilishwa na Mamlaka za udhibiti na vyombo vya ulinzi na usalama na utoaji wa ushahidi mahakamani baada ya uchunguzi kukamilika wakati Mhe. Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kutembelea banda la Mamlaka kabla ya kufunga Maadhimisho ya Siku ya Kitaifa ya Kupiga Vita Dawa za Kulevya, yaliyofanyika katika uwanja wa Sheikh Amri Abeid, jijini Arusha, Juni 25, 2023. Katikati ni Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa.***

# KAMISHNA JENERALI WA DAWA ZA KULEVYA AIPONGEZA GCLA

Na Sylvester Omary

Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Aretas Lyimo, ameipongeza Mamlaka ya Maabara ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kwa utoaji wa haraka wa ripoti za uchunguzi na uboreshaji wa mifumo ya utendaji kazi.

Kamishna Jenerali aliyasema hayo jijini Dodoma alipotembelea banda la Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kwenye maadhimisho ya Wiki ya Sheria yaliyofanyika katika viwanja vya Nyerere Square.

"Nawapongeza kwa kuwahisha ripoti za uchunguzi na kuendana na kasi ya Serikali ya awamu ya sita kwa kununua mitambo imara na yenye ubora katika uchunguzi wa kimaabara na kupata ithibati za mifumo ya kimataifa" alisema Kamishna Jenerali.

Aidha, Kamishna Aretas Lyimo, alipongeza Mamlaka kwa kuwa na mifumo ya taarifa za uchunguzi wa kimaabara na wa taarifa za mashahidi wataalam ambayo inasaidia kubadilisha taarifa na wadau wengine wa haki jinai.

"Nawapongeza pia kwa kuwa na mifumo ya kufanyia kazi ya kisasa, hii yote inasaidia kuongeza utendaji kazi na kusaidia vyombo vingine na Mahakama kwenye utendaji haki ili kuleta ustawi kwa Taifa" alisema.



*Mkemia Mkuu wa Serikali, Dkt. Fidelice Mafumiko (kulia) akimuelezea Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Aretas Lymo (katikati) namna uchunguzi wa kimaabara wa sampuli za Vinasaba vya Binadamu unavyofanyika mara baada ya Kamishna Jenerali kutembelea maabara ya Sayansi Jinai Baiolojia na Vinasaba iliyopo Mamlaka Makao Makuu, Dodoma Mei 20, 2024.*



*Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Boniphace Luhende (kushoto), akipata maelezo kutoka kwa Mkemia Mwandamizi kutoka Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Leticia Waitara (katikati), akielezia majukumu ya Mamlaka kwa alipotembelea banda la Mamlaka kwenye Maonesho ya Maadhimisho ya Wiki ya Sheria katika viwanja vya Nyerere Square, jijini Dodoma.*

# ALLERGY - UGONJWA UNAOKUA KWA KASI

Na Dkt. Kassim Babu Mapondela

Allergy au Mzio ni ugonjwa ambao kinga ya mwili ya binadamu inakinzana nao kuliko kawaida (hypersensitivity reaction) na baadhi ya vitu ambavyo ni vya kawaida kabisa katika maisha na mazingira ya binadamu, ambavyo kwa kundi kubwa la watu ni vitu visivyo na madhara kama vile protini kwenye aina tofauti ya vyakula na matunda, wadudu, dawa, poleni, fangasi na viambatanishi kwenye vyakula vilivyosindikwa (food additives and preservatives).

Kwa watu wenye tatizo la aleji/mzio kinga zao za mwili huona vitu hivi kama vya hatari na kupelekea kuzalisha kinga ya mwili zisizokuwa za kawaida. Tatizo hili ni la kurithi na huwapata watu wenye vinasaba hivi vya mzio (atopy tendence).

Allergy/mzio imegawanyika katika makundi makubwa mawili, kundi la kwanza ni mzio inayotokana na vitu vilivyomo kwenye hewa na mazingira ambavyo huathiri mfumo wa upumuaji zaidi, kwa mfano poleni za maua, majani na miti, fangasi, wadudu wanaoishi kwenye vumbi jepesi (house dust mites) wanyama kama vile paka, mbwa na ndege wakufugwa pamoja na mende. Pumu ya kifua, aleji ya pua na kwa kiasi fulani pumu ya ngozi ni mfano wa mzio zinazoweza kuchangiwa na mazingira. Kundi la pili ni allergy au mzio wa vitu tunavyokula (vyakula, matunda, dawa na viambatanisho vilivyomo kwenye vyakula na vinywaji vilivyosindikwa). Mzio huu huathiri zaidi mfumo wa chakula na ngozi.

Kwa miaka ya hivi karibuni tatizo la allergy au mzio limekua likiongezeka kwa kasi na takwimu zinaonyesha kuwa kwa nchi zilizoendelea kati ya watu kumi, wanne wana allegy na kwa nchi ya Tanzania kati ya watoto kumi wa shule za sekondari wawili wana changamoto ya mzio. Mojawapo ya sababu zinazohusishwa na ongezeko hilo ni kama mabadiliko ya tabia nchi na hali ya hewa, mabadiliko ya mfumo wa Maisha, ulaji wa vyakula visivyo hai (processed foods), watoto kutopendelea kucheza nje ya nyumba na kutumia muda mwingi kuwa ndani wakitazama runinga au kucheza michezo ya kwenye kompyuta, kutonyonya maziwa ya mama pamoja kujifungua kwa njia ya upasuaji.




Dalili za ugonjwa wa allergy au mzio ni kama kupiga chafya mfululizo, kuwashwa koo, pua, masikio na macho, mafua ya mara kwa mara, kubanwa kifua, kutoa sauti kama filimbi wakati wa kupumua, kikohozi cha mara kwa mara, maumivu ya tumbo,kutapika na kuharisha, kuvimba kwa midomo, ulimi, koo na masikio, viganja vya mikono, vipele vinavyowasha (hives and urticaria rashes) na wakati mwingine dalili huweza kuwa kubwa na kusababisha anaphylaxis. Dalili hizi hutokea punde tu mgonjwa anapokuwa amekutana au kutumia vitu vyenye asili ya mzio. Mara chache dalili hizi zinaweza kuwa kubwa na kupelekea hata kifo.

Mzio unaweza kuepukika au kuisha kama mgonjwa atapatiwa matibabu sahihi akiwa bado mtoto au wakati mzio unapojitokeza. Baadhi ya njia zilizothibitika kisayansi kusaidia kupunguza uwezekano wa kupata mzio ni kama zifuatazo;

- Mama anashauriwa kutumia kwa wingi vyakula vyenye asili ya aleji kama maziwa, karanga na mayai wakati wa ujauzito. Hii husaidia mtoto kuanza kuvizoea akiwa tumboni.
- Kujifungua kwa njia ya kawaida, hii husaidia mtoto kupata bakteria wazuri wa kutosha ambao huifunza kinga ya mwili na kuilekeza zaidi upande wa kupambana na maambukizi.
- Kunyonyesha mtoto angalau kwa miezi minne ya kwanza bila kumchanganyia na maziwa ya kopo. Njia hii husaidia ukuaji mzuri wa mtoto na kumjengea kinga ya mwili iliyokuwa kamili.
- Kupunguza kukutana na visababishi vya aleji au mzio. Kwenye hili tunashauriwa kuwapa watoto muda mwingi wa kucheza nje ya nyumba badala ya kutumia muda mwingi ndani ya nyumba wakitazama runinga na kucheza michezo ya kompyuta. Hili husaidia watoto kujenga kinga ya mwili ya magonjwa badala ya kinga mwili ya aleji.
- Njia ya mwisho ni kumpa mtoto vyakula vyenye asili ya aleji mapema baada ya muda wa miezi sita ya kunyonyesha maziwa peke yake kupita. Hii itasaidia mwili kutotambua protini zilizopo kwenye vyakula kama protini hatarishi na kuzishambulia kunakopelekea tatizo la aleji au mzio.

Aleji inatibika na mgonjwa mwenye aleji anashauriwa kuwahi hospitali, kituo cha afya au Zahanati ya karibu ili kuweza kupatiwa matibabu ya awali pamoja na elimu ya afya.

**Chapisho hili limeandaliwa na Dkt. Kassim Babu Mapondela**
**Daktari Bingwa wa magonjwa ya Allegy na Kinga Mwili - Hospitali ya Taifa Muhimbili na Mhadhiri Chuo Kikuu Cha Tiba na Afya - Muhimbili**
**0715870080**

# BARAZA LASISITIZWA KUSIMAMIA NIDHAMU YA KAZI KWA WAFANYAKAZI

**Na Okello Thomas**

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Profesa Esther Lugwisha, amevitaka vikao vya Baraza la Wafanyakazi vitumike kujadili na kuboresha malengo na mipango ya Taasisi na utekelezaji wake kwa lengo la kuongeza tija na ufanisi.

Profesa Esther Lugwisha aliyasema hayo wakati akifungua Kikao cha Tano cha Baraza la Sita la Wafanyakazi wa Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA), kilichofanyika kwenye ukumbi wa PSSF Commercial Complex jijini Dar es Salaam Februari 15, 2024.

"Madhumuni ya Msingi ya Baraza la Wafanyakazi ni kutoa fursa kwa watumishi kupitia wawakilishi wao kujadiliana juu ya masuala mbalimbali ya msingi yanayohusu tija, ufanisi na maslahi ya watumishi, na kuishauri Menejimenti juu ya masuala hayo. Aidha, Baraza la Wafanyakazi linawajibu mkubwa wa kuhakikisha kuwa, kunakuwepo na maelewano, ushirikiano na mshikamano kati ya wafanyakazi na Uongozi wa Taasisi", alisema Profesa Lugwisha.

Aidha, Mwenyekiti wa Bodi amevitaka vikao vya Baraza la Wafanyakazi vitumike kujadili na kuboresha malengo na mipango ya Taasisi kwa kuzingatia kuwa tija na ufanisi vinapoongezeka vinapaswa kwenda sambamba na ongezeko la Maslahi kwa Watumishi. Hivyo, majadiliano na ushauri ujikite kwenye kuongeza utendaji bora na wenye kuleta tija zaidi kwani tija inapoongezeka inapelekea urahisi wa kuomba nyongeza ya maslahi kwa watumishi ambayo hatimae yanawawezesha watumishi kuishi maisha bora zaidi. Pia, Profesa amesisitiza uwepo wa nidhamu ya kazi kwa wafanyakazi ambayo inachangia uendeshaji bora wa shughuli za Taasisi.

Sambamba na hilo, Mwenyekiti aliongeza kuwa Bodi inatambua umuhimu, unyeti, upana na ugumu wa majukumu na kazi zinazofanywa na Mamlaka katika kulinda Afya, usalama wa watu na mazingira na kuchangia katika upatikanaji wa haki kwenye vyombo vya maamuzi. Hivyo, Bodi inatambua mchango wa kila mtumishi wa Mamlaka katika uwajibikaji kwenye utekelezaji wa majukumu.



*Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka, Profesa Esther Lugwisha, akizungumza wakati akifungua Kikao cha Tano cha Baraza la Saba la Wafanyakazi wa Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA), kilichofanyika katika Ukumbi wa PSSSF Commercial Complex, jijini Dar es Salaam, Februari 15, 2024.*



*Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi la Mamlaka, Dkt. Fidelice Mafumiko (katikati), akizungumza wakati akiowaongoza Wajumbe wa kikao cha nne cha Baraza hilo linalojumuisha zaidi ya wajumbe 61. Kushoto ni Katibu wa Baraza la Wafanyakazi, Florida Tumbu, na kulia ni Katibu Msaidizi wa Baraza, Rotani Bugumba.*



*Picha ya chini: Mjumbe wa Baraza Victoria Kyara katika Kikao cha Tano cha Baraza la Saba la Wafanyakazi wa Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA).*

# MAMLAKA YANG'ARA MICHEZO YA SHIMMUTA

Na Okello Thomas



***Wanamichezo wa Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali wakishangilia baada ya kukabidhiwa kombe na medali kwenye Michezo ya Mashirika ya Umma, Taasisi na Makampuni Binafsi Tanzania (SHIMMUTA), yaliyofanyika kuanzia Novemba 12 hadi 26, 2023 jijini Dodoma.***

Wanamichezo wa Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA), wameng'ara katika Michezo ya Mashirika ya Umma, Taasisi na Makampuni BinafsiTanzania (Shimmuta 2023), yaliyofanyika kuanzia Novemba 12 hadi 26, 2023 jijini Dodoma, baada ya kufanya vizuri katika mbio za magunia na riadha.

Katika mashindano hayo, Mamlaka imeibuka mshindi wa pili kwenye mchezo wa mbio za gunia, mshindi wa pili kwenye riadha (wanawake) mita 800 na mshindi wa tatu kwenye riadha (wanawake) mita 5000.

Akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi wa Huduma za Taasisi, Makamu Mwenyekiti wa Michezo GCLA, Sabas Mandari alibainisha kuwa ushindi huo ni uthibitisho kuwa uongozi wa Mamlaka unathamini michezo, hivyo kuwezesha watumishi kushiriki mashindano ya Shimmuta. Pia, amempongeza Mkemia Mkuu wa Serikali Dkt. Fidelice Mafumiko kwa ushirikiano wake katika kuhakikisha michezo inapewa kipaumbele.

"Nichukue nafasi hii kumshukuru Mkemia Mkuu wa Serikali ambaye amekuwa nasi bega kwa bega kuanzia wakati wa maandalizi, wakati wa safari na kutupokea Dodoma pamoja na kutupa hamasa," alisema Mandari.

Aidha, Makamu Mwenyekiti amemshukuru Mkurugenzi wa Huduma za Taasisi Evaclotida Kapinga kwa mchango wake kwa wanamichezo wa Mamlaka ikiwa na yeye mwenyewe mwanamichezo ambaye alijitahidi kutupa hamasa ya kutupa moyo, pia alicheza kwa kujituma licha ya kwamba ni kiongozi.

Aidha, amewapongeza wanamichezo kwa namna walivyojitoa muda wote wa mashindano mpaka mwisho na kuwasihi kutokata tamaa kwani anaamini mwakani wanamichezo wa Mamlaka watafanya mambo makubwa zaidi na kupaisha jina la taasisi.

Mandari, alitoa rai kwa watumishi wa Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kuchukulia michezo kama ni ya kila mmoja kwani michezo ni urafiki, michezo ni afya na kupitia michezo kila mmoja anaweza kuboresha utendaji wake wa kazi.

Kadhalika, amewashukuru watumishi wa Mamlaka waliopo Dodoma kwa kuonesha upendo kama familia moja ya GCLA kwa kufika kwenye viwanja mbalimbali kushangilia timu za Mamlaka zilipokuwa zikicheza.

Katika mashindano hayo, timu ya mpira wa pete ya Mamlaka kwa mara ya kwanza ilifanikiwa kuingia katika hatua ya 16 bora.



***Makamu Mwenyekiti wa Michezo GCLA, Sabas Mandari (kulia), akiwa na kombe la mshindi wa pili kwenye mchezo wa mbio za gunia.***

# MKEMIA MKUU WA SERIKALI AHIMIZA UADILIFU MAHALA PA KAZI

Na Sylvester Omary

Mkemia Mkuu wa Serikali Dkt. Fidelice Mafumiko, amewataka Watumishi wa Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Kanda ya Kaskazini – Arusha kufuata misingi, kanuni, taratibu na kufanya kazi kwa uadilifu na kuzingatia maadili ya utumishi wa umma ili kuongeza tija katika kuwahudumia wananchi.

Dkt. Mafumiko alitoa wito huo Disemba 8, 2023, wakati akifungua kikao maalum cha Uadilifu kwa Watumishi wa Mamlaka kilichofanyika katika Ofisi ya Kanda ya Kaskazini.

Dkt. Mafumiko amewataka watumishi wa Mamlaka kuzingatia uadilifu ili watekeleze majukumu waliyokabidhiwa kama dhamana ya kuhudumia umma bila upendeleo na kuweka jitihada katika kuhakikisha watumishi wanajenga umahiri kwani utaongeza fursa za maendeleo binafsi.

"Uadilifu ni uwezo wa mtumishi kutenda anayopaswa kutenda na kutotenda asiyopaswa kutenda kwa kujisimamia yeye mwenyewe. Mambo ambayo mtumishi hapaswi kuyatenda ni pamoja na kupokea rushwa, kuchelewa kufika kazini au kutofika kabisa kazini kwa visingizio vya uongo, kutoa huduma kwa upendeleo kwa wateja wa ndani na nje, kutomaliza kazi kwa wakati, kutoa taarifa za uongo, kujihusisha na mahusiano ya kimapenzi mahali pa kazi na mengine," alisisitiza Dkt. Mafumiko.

Katika hatua nyingine Mkemia Mkuu wa Serikali ameridhia Kamati ya Uadilifu kuanzisha utaratibu wa kuwaelimisha watumishi wa Mamlaka ili kuendelea kuwajengea uwezo watumishi kuhusu masuala ya maadili.

Naye, Meneja wa Ofisi ya Kanda ya Kaskazini Eliamini Mkenga, ameishukuru Kamati ya Uadilifu kutoa mafunzo kwa watumishi wa Kanda hiyo, hivyo wategemee kuongezeka kwa uadilifu na umahiri wa hali ya juu kutoka kwa watumishi wa Kanda ya kaskazini katika utekelezaji wa majukumu yao. Vilevile,

Mkenga aliwapongeza watumishi wa Kanda kwa ueledi na utendaji kazi mzuri katika utekelezaji wa majukumu yao ambayo unachangia katika ukuaji wa taasisi.



*Mkemia Mkuu wa Serikali, Dkt. Fidelice Mafumiko (aliyesimama), akizungumza na Wajumbe wa Kamati ya Uadilifu na watumishi wa Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali Ofisi ya Kanda ya Kaskazini wakati akifungua mafunzo ya uadilifu na maadili mahala pa kazi. Mafunzo hayo yaliyofanyika katika ofisi ya Kanda ya Kaskazini - Arusha Disemba 8, 2023.*



*Viongozi wa Mamlaka, Wajumbe wa Kamati ya Uadilifu pamoja na Watumishi wa Kanda ya Kaskazini wakifuatilia hotuba ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Dkt. Fidelice Mafumiko (hayupo pichani) wakati akifungua mafunzo hayo jijini Arusha.*

*"Uadilifu ni uwezo wa mtumishi kutenda anayopaswa kutenda na kutotenda asiyopaswa kutenda kwa kujisimamia yeye mwenyewe. Mambo ambayo mtumishi hapaswi kuyatenda ni pamoja na kupokea rushwa, kuchelewa kufika kazini kwa visingizio vya uongo, kutoa huduma kwa upendeleo kwa wateja wa ndani na nje, kutoa taarifa za uongo, kujihusisha na mahusiano ya kimapenzi mahali pa kazi na mengine"*

***DKT. FIDELICE MAFUMIKO***
***Mkemia Mkuu wa Serikali***

# WANAWAKE WA GCLA WATOA MSAADA KITUO CHA WATOTO YATIMA

Na Okello Thomas

Watumishi wanawake kutoka Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA), wameadhimisha siku ya kimataifa ya wanawake duniani kwa kutoa msaada wa katika kituo cha kulelea watoto yatima cha Sarah House kilichopo Mwandege,Mkoa wa Pwani.

Akizungumza baada ya kuwasilisha msaada huo kwa uongozi wa kituo hicho, Mwenyekiti wa wanawake wa Mamlaka, Veronica Chiligati alisema kuwa katika kuadhimisha siku ya wanawake duniani, wameona ni vyema kurudisha shukrani kwa jamii kwa kutembelea watoto yatima zaidi ya 90 wanaoishi katika kituo hicho kilichopo Mwandege mkoani Pwani Februari 26, 2024.

“Niwashukuru watumishi wote wa Mamlaka kwa michango yao ya hali na mali, lakini napenda kuwasihi kuendelea na moyo wa kutoa ili watoto wetu wajione kuthaminiwa katika jamii. Pia tunamshukuru Mkemia Mkuu wa Serikali, Dkt. Fidelice Mafumiko kwa kutoa ushirikiano pamoja na kuwa mstari wa mbele katika kuhamasisha zoezi hilo,” alisema Chiligati.

Naye, msimamizi wa kituo kulelea wa yatima cha Sarah House, Stella Kishekwa aliwashukuru watumishi wa Mamlaka kwa moyo wa kutoa na kuguswa na maisha ya watoto wa kituo hicho kwani kwa walichokitoa kinawapa faraja na matumaini watoto hao.

"Tumefurahi sana kupokea msaada huu kutoka kwa wanawake wa Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, tumefarijika sana sisi kama walezi na watoto kupokea msaada wa vitu hivi ambavyo wototo wengi hawakuwa navyo. Mungu awabariki sana na tunaamini mlicho kianzisha kitaendelea ili watoto wetu waweze kufikia malengo yao,” alisema Kishekwa.

Baadhi ya vitu ambavyo wametoa katika kituo hicho ni pamoja na vitambaa vya sa za shule, madaftari, nguo, viatu, taulo za kike, vyakula na vingine mbalimbali.




*Mwenyekiti wa Wanawake wa Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Veronica Chiligati (kulia), akimkabidhi vitambaa vya sare za shule Stella Kishekwa ambaye ni mlezi wa watoto yatima wa kituo cha Sarah House, kilichopo Mwandege Februari 26, 2024.*



*Afisa Ustawi wa Jamii wilaya ya Mkuranga, Abigail Ngasa (kushoto), akitoa neno la shukrani kwa wageni kutoka Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, baada ya kupokea msaada wa vitu mbalimbali kutoka kwa watumishi wa Mamlaka.*

# GCLA YAPONGEZWA KWA KUTOA RIPOTI ZA UCHUNGUZI KWA WAKATI



*Jaji wa Mahakama Kuu, Kanda ya Dar es Salaam, Mhe. David Ngunyale (kushoto) akipata maelezo juu ya majukumu yanayotekelezwa na Mamlaka katika uchunguzi wa kimaabara wa sampuli za makosa ya jinai kutoka kwa mtumishi wa Mamlaka Muhsin Kilonzo (kulia) kwenye Maadhimisho ya Wiki ya Sheria yaliyofanyika katika viwanja vya Mnazi Mmoja Dar es Salaam Januari 24, 2024.*

Na Mwanaheri Jazza

Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali imepongezwa kwa kuimarisha utoaji wa ripoti za uchunguzi wa kimaabara za mashauri mbalimbali kwa muda mfupi.

Pongezi hizo zilitolewa na Jaji wa Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam, Mhe. David Ngunyale alipotembelea banda la Mamlaka katika maadhimisho ya Wiki ya Sheria, Kanda ya Dar es Salaam ambapo amesema utoaji wa ripoti za uchunguzi wa vinasaba kwa sasa umeimarika tofauti na hapo zamani.

"Hongereni sana utoaji wa ripoti za uchunguzi wa vinasaba kwa sasa umeimarika sana, kwa sasa ripoti zinatoka mapema ukilinganisha na hapo zamani. "alisema Jaji Ngunyale.

Kwa upande wake Jaji Mfawidhi Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam, Mhe. Salma Maghimbi, ameipongeza Mamlaka kwa utendaji kazi uliotukuka huku akiishukuru Mamlaka kwa ushiriki wake katika maadhimisho hayo kama wadau muhimu katika mnyororo wa haki.

"Hongereni sana kwa kazi nzuri na nzito mnayoitoa kwa jamii na tunawashukuru sana kwa ushirikiano wenu katika maadhimisho haya"alisema Jaji Maghembe.

Maadhimisho ya Wiki ya sheria yalianza rasmi Januari 24, 2024 na kuhitimishwa Februari 1, 2024.

## UTOAJI WA ELIMU YA KEMIKALI KWA WADAU NI TAKWA LA KISHERIA

Na Okello Thomas

Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA), kupitia Ofisi ya Kanda ya Kati - Dodoma imetoa mafunzo kwa wasimamizi wa kemikali kwa lengo la kuhakikisha wanawasimamia vyema shughuli mbalimbali za kemikali katika maeneo yao ya kazi.

Akizungumza wakati akifungua mafunzo hayo jijini Dodoma leo, Mkurugenzi wa Huduma za Udhibiti, Daniel Ndiyo, alieleza kuwa dhumuni la kutoa mafunzo hayo ni kutokana na matakwa ya Sheria ya Kemikali ya Viwandani na Majumbani Sura 182, ambayo inataka wadau wote wanaojishughulisha na kemikali kuwa na uelewa wa matumizi sahihi na salama ya kemikali.

"Matumizi ya kemikali huzalisha kemikali taka ambazo zinaweza kuleta madhara kwa afya na mazingira zisipodhibitiwa, hivyo mafunzo haya ni muhimu katika kujenga uelewa wa kujihusisha na kemikali pamoja na kuzuia ajali zinazoweza kutokea kutokana na matumizi yasiyo sahihi na salama ya kemikali," alisema Ndiyo.

Aidha, Mkurugenzi aliongeza kuwa mafunzo hayo yatawajengea uwezo wasimamizi wa kemikali katika kujua madhara na faida ya kemikali na wote wanatakiwa kujua namna sahihi ya kutumia kemikali na kushughulikia kemikali-taka zinazozalishwa kwani ajali mbalimbali za kemikali hutokana na sababu kadhaa, zikiwemo uelewa mdogo wa sheria za nchi na ufinyu wa rasilimali watu, hivyo kuchangia matumizi ya kemikali yasiyo sahihi na udhibiti hafifu wa kemikali taka.

Naye, Meneja wa Ofisi ya Kanda ya Kati – Dodoma, Gerald Meliyo, ametoa rai kwa wasimamizi wa kemikali kuhakikisha wanakuwa kwenye nafasi chanya ya kuwaelimisha wafanyakazi waliopo chini yao na pia kuwa mabalozi wa kuhamasisha wadau wengine kupata mafunzo pamoja na kueneza elimu ya matumizi salama ya kemikali katika maeneo yao ya kazi na nje ili kulinda afya za watu, wanyama na mazingira........*Inaendelea Uk. 24*

Inatoka Uk. 23

Kwa upande wake mshiriki wa mafunzo Mhandisi. Aron Mwaigaga, ameishauri Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, kuendela kutoa elimu kwa wadau na wananchi kwa kuwaalika lakini pia kuwafikia katika maeneo yao ya kazi kwani elimu itawafikia wengi zaidi kutokana na maeneo ya kazi kuwa na wahusika wengi kwa wakati mmoja.
Mafunzo hayo ya usimamizi salama wa kemikali yanahusisha washiriki zaidi ya 80 kutoka mikoa ya Iringa, Tabora, Singida, Dodoma na Morogoro yatafanyika kwa siku tatu kuanzia Januari 24 hadi 26, 2024, jijini Dodoma.



***Mkurugenzi wa Huduma za Udhibiti, Daniel Ndiyo (aliyekaa katikati), akiwa pamoja na washiriki wa mafunzo kutoka mikoa mbalimbali, viongozi kutoka Mamlaka pamoja na watumishi wa Mamlaka. Kuanzia kushoto waliokaa, ni Meneja wa Ofisi ya Kanda ya Kati – Dodoma, Gerald Meliyo na kulia ni Meneja wa Usajili wa Kemikali na Maabara za Kemia, Musa Kuzumila. Aliyesimama kushoto ni Msimamizi wa Fedha na Utawala wa Ofisi ya Kanda ya Kati, Cosmas Makolobelah.***

# TANZANIA IPO TAYARI KUKABILIANA NA MAAFA YA KIKEMIKALI NA KIMIONZI

**Na Okello Thomas**

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa amesema Serikali kwa sasa ipo tayari kuhakikisha usalama wa nchi dhidi ya majanga, maafa na dharura mbalimbali zikiwemo za kikemikali, kibaiolojia, kimionzi na kinyuklia.

Mhe. Kassim Majaliwa, alitoa kauli hiyo Machi 14, 2024 wakati wa ufungaji wa mafunzo ya zoezi la utayari dhidi ya dharura za kikemikali na kimionzi Tanzania yaliyofanyika katika viwanja vya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji bandarini jijini Dar es Salaam.

Aidha, Waziri Mkuu amezitaka wizara na taasisi zote zinazohusika na kutekeleza mipango hiyo kuitumia kikamilifu na zitoe ushirikiano kwa wote wanaohitaji kutekeleza miongozo hiyo na pia kukamilisha maandalizi ya nyaraka mbili muhimu za Mpango wa Kitaifa wa Maafa ya Kikemikali, Kibaiolojia, Kiradiolojia na Kinyukilia (CBRN National Action Plan), na Mpango wa Kuitikia wakati wa Dharura za Kinyuklia na Kiradiolojia (Radiological and Nuclear Response Plan) ambazo alizizindua katika hafla hiyo.

"Kupitia nyaraka hizi, mmeweka mikakati ya pamoja ya kitaifa ya namna ya kukabiliana na kujikinga na majanga yatokanayo na dharura za kikemikali, kibaiolojia, kimionzi na kinyuklia. Hivyo nimefurahi sana kusikia nyaraka hizo zimezingatia masuala muhimu ya kisera, uzoefu wa kukabiliana na majanga kitaifa na kimataifa pamoja na matakwa ya kisheria na itifaki za kimataifa," alisema Mhe. Majaliwa.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Nguvu za Atomu, Profesa Lazaro Busagala alisema kuwa umuhimu wa zoezi hilo ni kuhakikisha kwamba inapotokea dharura ya kibaiolojia, kikemikali na kimionzi, timu ya wataalam inahakikisha kuwa usalama unakuwepo na pia kuokoa maisha ya watu pamoja na mali.

Naye, Mkemia Mkemia Mkuu wa Serikali Dkt. Fidelice Mafumiko amesema kuwa mazoezi ya utayari dhidi ya dharura za kikemikali na kimionzi yataendelea kufanyika mara kwa mara kwa lengo la kujenga utayari wa timu ya Taifa ya kujiandaa na kukabiliana na dharura za kitaifa.

## HABARI PICHA



Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa akizungumza wakati akizindua zoezi la utayari dhidi ya dharura za kikemikali na kimionzi Tanzania (ZOKIKITA 2024). Hafla hiyo ilifanyika katika viwanja vya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji bandarini, jijini Dar es Salaam Machi 14, 2024.




Wataalam kutoka Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA), Ibrahim Kinganije (kushoto) na Placida Kabelege (kulia) wakichukua sampuli katika eneo la ajali ya kemikali kwenye Maonesho ya ZOKIKITA yaliyofanyika katika viwanja vya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji katika Bandari ya Dar es Salaam Machi 14, 2024.

# KATIBU MKUU AZINDUA KAMATI YA KITAALAM YA VINASABA VYA BINADAMU

**Na Mwanaheri Jazza**

Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Dkt. John Jingu, ameipongeza Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kwa kuunda Kamati ya kitaalamu ya Vinasaba vya Binadamu ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Sheria ya Vinasaba vya Binadamu Sura ya 73.

Dkt Jingu ametoa pongezi hizo jijini Dodoma wakati akizindua Kamati hiyo na kusema kuwa ana imani itasaidia Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali katika kutimiza wajibu wake kwa nchi na Serikali na kuendeleza mahusiano mema na Taasisi ambazo zina majukumu yanayoshabihiana.

"Ni matumani yangu kuwa kamati tunayoizindua hii leo itasaidia Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali katika kutimiza wajibu wake kwa nchi na Serikali, lakini pia itaendeleza mahusiano mema ya kiutendaji kati ya Mamlaka hii na taasisi ambazo zina majukumu yanayoshabihiana" alisema Dkt Jingu.

Dkt Jingu pia ametoa rai kwa kamati hiyo hasa kwa wanaofanya uchunguzi wa Vinasaba vya Binadamu kufuata maadili ya kazi na kutumia teknolojia za kisasa ili kuepuka madhara au migogoro inayoweza kujitokeza.

"Masuala ya Vinasaba yana mambo mengi ambayo yanaweza kuisaidia jamii, lakini pia yanahitaji kiwango kikubwa cha kimaadili na kiusimamizi, lakini pia ili muweze kufanya kazi vizuri ni muhimu na ni lazima mjihakikishie mnakwenda sambamba na mabadiliko ya teknolojia ya vinasaba duniani kwa kuwa inabadilika kwa haraka sana" alisema Dkt Jingu.

Kwa upande wake Mkemia Mkuu wa Serikali, Dkt Fidelice Mafumiko, ametaja majukumu yanayofanywa na Mamlaka ikiwemo sheria ya Udhibiti Matumizi ya Vinasaba vya Binadamu sura ya 73.

"Chini ya sheria hii Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali inapata kusajiri na kukagua wadau wa maabara zinazojishughulisha na uchunguzi wa Vinasaba vya Binadamu nchini kwa lengo la kuweza kudhibiti matumizi mabaya ya taarifa za vinasaba, kwa mujibu wa sheria hii Mamlaka pia imepewa jukumu la kutoa vibali vya kufanya utafiti wa suala linalohusisha Vinasaba vya Binadamu" alisema Dkt. Mafumiko.

Nae, Mganga Mkuu wa Serikali, Dkt. Tumaini Nagu, ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kamati hiyo, ameahidi kupokea maelekezo yote yaliyoainishwa kwenye kamati hiyo na kuyatekeleza kwa mujibu wa sheria, kanuni na miongozo iliyopo.

"Kwa niaba ya wenzangu wote wajumbe wa kamati hii ya kitaalamu ya vinasaba tunasema tumepokea maelekezo yote, kuhusu unyeti wa kazi hii, lakini pia kuhusu mabadiliko ya teknolojia ambayo yanaenda kwa kasi sana na vilevile maelekezo kuhusu masuala ya ustawi wa jamii na usalama wa watu wenyewe na usalama wa nchi na kuhakikisha kwamba haki inapatikana kwa wakati na inazingatiwa. Niseme tu kuwa tumepokea na sisi tunaahidi tutatimiza kazi yetu kwa kuzingatia sheria, kanuni na miongozo" alisema Dkt. Nagu.





*Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Dkt. John Jingu (kulia), akikabidhi begi lenye nyaraka za kutendea kazi kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kitaalam ya Vinasaba vya Binadamu, Profesa Tumaini Nagu, wakati wa uzinduzi wa Kamati ya Kitaalam ya Vinasaba vya Binadamu (Human DNA Technical Committee) katika ofisi za Makao Makuu ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali jijini Dodoma, Mei 6, 2024.*

*"Ni matumani yangu kuwa kamati tunayoizindua hii leo itasaidia Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali katika kutimiza wajibu wake kwa nchi na Serikali, lakini pia itaendeleza mahusiano mema ya kiutendaji kati ya Mamlaka hii na taasisi ambazo zina majukumu yanayoshabihiana"*

*Dkt John Jingu - Katibu Mkuu Wizara ya Afya*

# WATAALAM WATAKIWA KUWASAIDIA WANANCHI

**Na Judith Lema**

Mkuu wa Wilaya ya Kisarawe Mhe. Fatma Nyangasa, amesema kuwa Serikali inatumia fedha, muda na raslimali watu kuhakikisha kuwa wananchi wake wanaelimika na kupata uelewa wa pamoja juu ya shughuli inazozitekeleza.

Mhe. Nyangasa aliyasema hayo Machi 4, 2024 wakati akifungua mafunzo ya Utekelezaji wa Sheria za Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kwa viongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe Mkoa wa Pwani.

"Mafunzo haya ya Utekelezaji wa sheria za Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali yametusaidia sana kwani kabla ya hapo hatukuwa na uelewa mzuri juu ya kazi zinazofanywa na Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali. Sisi tunapata kesi nyingi za Watoto waliobakwa na nyinginezo, hivyo kupitia mafunzo haya tumeona hakuna sababu ya kushindwa kumsaidia mwananchi wa kawaida kwa kutokujua taratibu" alisema.

Hata hivyo, Mhe. Mkuu wa Wilaya amemshukuru na kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa anayofanya ya kuboresha mazingira ya utendaji kazi kwa kuwezesha Mamlaka kununua mitambo ya kisasa ya gharama kubwa na hivyo kurahisisha utendaji kazi na upatikanaji wa haki kwa wakati.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Huduma za Ubora wa Bidhaa na Mazingira, kutoka Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Sabanitho Mtega, alibainisha kuwa Mamlaka imekuwa ikitoa mafunzo kwa wadau na watumishi wa Serikali ambao wanashirikiana nao katika shughuli mbalimbali.

"Ni vibaya sana kudhani kila mmoja anajua majukumu unayofanya, lakini kwa mafunzo haya yatasaidia kujua Mamlaka inafanya nini na huduma gani zinatolewa, na wapi wanakoweza kuzipata" alisema Mtega.

Mbali na mafunzo hayo Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, pia imetoa vitakasa mikono (Sanitizer) na kuvikabidhi kwa uongozi wa Halmashauri hiyo ili vitumike katika kuwasaidia kujikinga na maambukizi mbalimbali.

"Ni vibaya sana kudhani kila mmojaanajua majukumu unayofanya, lakini kwa mafunzo haya yatasaidia kujua Mamlaka inafanya nini na huduma gani zinatolewa, na wapi wanakoweza kuzipata" alisema Mtega.

Mbali na mafunzo hayo Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, pia imetoa vitakasa mikono (Sanitizer) na kuvikabidhi kwa uongozi wa Halmashauri hiyo ili vitumike katika kuwasaidia kujikinga na maambukizi mbalimbali.




***Mkuu wa Wilaya ya Kisarawe, Mhe. Fatma Nyangasa (aliyekaa katikati) akiwa na wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya, Wakuu wa Idara na Vitengo wa Halmashauri ya Kisarawe, mara baada ya kukamilika kwa mafunzo ya Utekelezaji wa Sheria za Mamlaka yaliyofanyika katika ukumbi wa mikutano wa Kisarawe, Mkoa wa Pwani, Machi 4, 2024.***



***Meneja wa Ofisi ya Kanda ya Mashariki, Danstan Mkapa (aliyesimama) akizungumza wakati wa mafunzo kwa Wakuu wa Idara na Vitengo wa Halmashauri ya Kisarawe yanayofanyika Kisarawe, Mkoa wa Pwani.***

# WAJASIRIAMALI WAASWA MATUMIZI SALAMA YA KEMIKALI

**Na Jackson Monela**

Wajasiriamali wadogo na kati wanaozalisha bidhaa mbalimbali zinazotokana na Kemikali mkoani Tanga, wametakiwa kutumia kemikali hizo kwa usalama ili zisiweze kuleta madhara pindi wanapokuwa wakizitumia, kwani endapo zitatumika bila kuzingatia usalama, zinaweza kusababisha madhara makubwa kwa binadamu na kuleta athari katika mazingira.

Mkuu wa Wilaya ya Tanga, Joseph Kaji, aliyasema hayo wakati wa akifungua mafunzo ya matumizi salama ya kemikali kwa wajasiriamali hao yaliyoandaliwa na Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Kanda ya Kaskazini, kwa kushirikiana na SIDO Mkoa wa Tanga.

"Kemikali ni nzuri ukiitumia vizuri ila ukiitumia vibaya ina madhara makubwa. Kemikali mkiitumia vizuri itawanyanyua ila mkifanya mchezo ni hatari, nawaomba ,sikilize kwa makini mafunzo hay ana mkitoka hapa mkawe mabalozi wazuri kwa wajasiriamali wenzenu ambao wanatumia kemikali, wafikishieni elimu hii mtakayopatiwa", alisema Kaji.

Kwa upande wake Meneja wa Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali Kanda ya Kaskazini, Eliamini Mkenga, alisema lengo la mafunzo hayo ni kuwafundisha Wajasiriamali wadogo na wa kati namna sahihi ya matumizi salama ya kemikali, kuzalisha salama na kuhakikisha kila anayezungukwa na wazalishaji hao anakuwa salama dhidi ya madhara yanayoweza kuletwa na kemikali.

"Kila mtu ana haki ya kujua aina ya kemikali anayoitumia, kwa kujua madhara yake, namna ya kujikinga lakini pia atahadhalishe jamii yake namna ya kujikinga na kutumia kwa kuzingatia usalama. Hivyo mafunzo hayo ni muhimu kwa Wajasiriamali hawa na lazima tufahamu kemikali ni rafiki lakini kuna muda si rafiki na unatakiwa kuwa nayo makini", alisema Mkenga

Aidha, Mkenga alisema mafunzo hayo ambayo yanatolewa na Mamlaka hiyo ni muhimu kwa Wajasiriamali wanaotumia kemikali na sio kuyadharau, kwani yakitumika vizuri yatasaidia wajasiriamali hao kuweza kusonga mbele zaidi na hata kufikia kuwa wazalishaji wakubwa na si wadogo au kati.

Naye Meneja wa Shirika la Kuhudumia Viwanda vidogo (SIDO) Mkoa wa Tanga, Niko Mahinya, alisema kuwa mafunzo hayo si muhimu tu kwa wazalishaji hao, bali yanasaidia kuwakinga hata watumiaji wa bidhaa zitakazolishwa na wajasiriamali hao, kwani wataweza kuzalisha bidhaa ambazo zitakuwa salama na ambazo haziwezi kuwadhuru watumiaji wa bidhaa hizo.

Zaidi ya Wajasiriliamali wadogo na kati zaidi 150 kutoka Halmashauri mbalimbali za Mbalimbali za Mkoa wa Tanga, wameweza kushiriki kwenye mafunzo hayo ya siku mbili ya matumizi salama ya kemikali ambayo yameandaliwa na Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Kanda ya Kaskazini kwa kushirikiana na SIDO.



***Wajasiriamali wadogo na kati zaidi ya 50 wanaojihusisha na uzalishaji wa bidhaa kutokana na kemikali maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Tanga, wakifuatilia mafunzo ya usimamizi salama wa kemikali kutoka kwa Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kanda ya Kaskazini (GCLA), mafunzo ambayo yalilenga kuwajenga uwezo katika usimamizi salama wa kemikali pindi wanapokuwa kwenye uzalishaji wa bidhaa zao.***




***Mkuu wa Wilaya ya Tanga, Mhe. Joseph Kaji (aliyekaa katikati) akiwa pamoja na wawakilishi wa Wajasiriamali wadogo na kati wa Mkoa wa Tanga, wanaotumia kemikali kuzalisha bidhaa mbalimbali mara baada ya kufungua mafunzo kwa Wajasiriamali hao yaliyoandaliwa na GCLA Ofisi ya Kanda ya Kaskazini kwa kushirikiana na SIDO Mkoa wa Tanga, Mei 15 – 16, 2024. Aliyekaa kulia ni Meneja wa Ofisi ya Kanda ya Kaskazini, Eliamini Mkenga na kushoto ni Meneja wa SIDO Mkoa wa Tanga , Niko Mahinya.***

# GCLA YAWAJENGEA UELEWA WAANDISHI WA HABARI JUU YA MADHARA YA SUMU YA MADINI YA RISASI

**Na Judith Lema**

Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kupitia Kituo chake cha Kudhibiti Matukio ya Sumu imefanya mkutano na Waandishi wa Habari ili kuwajengea uelewa zaidi juu ya Udhibiti wa Madhara yatokanayo na sumu ya madini ya risasi.

Mkutano huo uliofanyika kwa kushirikiana na Asasi isiyo ya kiserikali ya Agenda ulilenga kuwakutanisha wadau wanaohusiana na uzalishaji rangi ambapo ni sehemu moja wapo ya upatikanaji wa sumu ya madini ya risasi na vyombo vya habari.

Akizungumza wakati wa ufunguzi wa mkutano huo, Mkuu wa Kituo cha kuratibu Matukio ya Sumu nchini, Yohana Goshashy, alisema kuwa sumu ya Madini ya risasi yana athari kubwa kwa maisha ya binadamu kwa kuwa yanapelekea mfumo wa fahamu na mfumo wa uzazi kuharibika pamoja na kusababisha ugonjwa wa kupooza.

"Madhara ya madini haya ni makubwa sana lakini uelewa wa wananchi bado sio mkubwa kiasi hicho, ndio maana sisi kama Kituo cha Kuratibu Matukio ya Sumu ambacho kipo Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali tumeungana na Asasi ya Agenda ili kupeleka msukumo na ujumbe huu kwa wananchi kuweza kujua kwamba kuna matukio yanayohusiana na sumu ya risasi ambayo hatuwezi kuona mara moja madhara yake kwa kuwa sumu hii ni moja ya sumu ambayo madhara yake yanachukuwa muda mrefu kuonekana," alisema Goshashy.

Aliongeza kuwa makundi makubwa yanayoathirika kwa kiasi kikubwa ni kundi la akina mama na Watoto. Hata hivyo amebainisha sababu mbalimbali zinazopelekea kuwepo kwa sumu ya madini ya risasi nchini kuwa ni pamoja na matumizi ya bidhaa zenye madini ya risasi ikiwa ni pamoja na midoli ya kuchezea watoto, uchakataji wa betri za magari na ardhi ambayo imeathiriwa inaweza kuwa chanzo kimojawapo cha uzalishaji wa madini ya risasi.

Akisisitiza umuhimu wa elimu kwa jamii, Goshashy alisema uelewa kwa wananchi bado ni mdogo, hivyo Mamlaka kwa kushirikiana na Asasi za Serikali na zisizo za Serikali imeona ni vyema kutoa elimu kwa vyombo vya habari ambavyo vinaweza kuwafikia wananchi wengi kwa muda mfupi na kwa upana mkubwa.

Kwa upande wake Dorah Swai, Afisa Programu kutoka Agenda, ametoa wito kwa Serikali kuongeza nguvu katika kupiga vita matumizi ya rangi zenye madini ya risasi, ikizingatiwa kuwa kiasi kikubwa cha madhara hayo yapo katika nchi zinazoendelea




***Mkuu wa Kituo cha Taifa cha Kudhibiti Matukio ya Sumu, Yohana Goshashy (katikati) akiongea na waandishi wa habari (hawapo pichani) katika mkutano wa kutoa uelewa juu udhibiti wa sumu ya madini ya risasi. Mkutano huo ulifanyika Oktoba 24, 2023 jijini Dar es Salaam, ikiwa ni katika kuadhimisha Wiki ya Kudhibiti Sumu ya Madini ya Risasi ambayo huadhimishwa katika wiki ya tatu ya mwezi Oktoba kila mwaka. Wengine kutoka kushoto ni Afisa Programu Mkuu, Silvani Mng'anya na Afisa programu, Dorah Swai, kutoka kutoka Asasi isiyo ya Serikali ya Agenda.***



***Baadhi ya waandishi wa habari wakimsikiliza Mkuu wa Kituo cha Taifa cha Kudhibiti Matukio ya Sumu, Yohana Goshashy (hayupo pichani) akiongea kwenye mkutano wa maadhimisho ya wiki ya Udhibiti sumu ya Madini ya risasi.***

# DKT. JINGU ATAKA WATAALAM WA TIBA ASILI NA TIBA MBADALA KUWEZESHWA

**Na Okello Thomas**

Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Dkt. John Jingu ametoa wito kwa Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA), kuwajengea uwezo wataalam wa tiba asili na tiba mbadala ili waweze kutoa huduma iliyo bora na salama kwa jamii.

Dkt. Jingu alitoa wito huo alipotembelea Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Ofisi ndogo ya Dar es Salaam Mei 27, 2024 ambapo alitembelea maabara ya Sayansi Jinai Baiolojia na Vinasaba.

Katibu Mkuu amewataka wataalam kutoka Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kufanya kazi kwa bidii na ubunifu ili kuweza kuwasaidia wataalam wa tiba asili na tiba mbadala na wadau wengine kwani wana imani kubwa na taasisi hii ya Mamlaka.

"Ili wataalam wa tiba asili na tiba mbadala waweze kufanya kazi vizuri ni lazima wafanye kazi na Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, hivyo ni jukumu letu sote kama wizara na taasisi kuhakikisha wataalam hawa wanawezeshwa kwa kuwapa elimu na kuchunguza bidhaa zao ili waweze kuzalisha kwa ufanisi na kiutaalam bila kuathiri afya za wananchi," alisema Dkt. Jingu.

Pia, Katibu Mkuu ametoa rai kwa Mamlaka kuhakikisha inasimamia vyema uzalishaji wa bidhaa mbalimbali nchini zinazotumia kemikali ili kuendelea kulinda usalama wa wananchi lakini pia kuzalisha bidhaa ambazo zitakubalika katika soko la kimataifa kupitia ubora.

Sambamba na hilo, Dkt. Jingu ameipongeza Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kwa kazi nzuri katika mnyororo mzima wa haki jinai nchini kwani Mamlaka inasaidia sana Mamlaka zinazohusika na haki jinai zikiwemo Jeshi la Polisi na Mahakama kwenye kutoa haki.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Huduma za Sayansi Jinai, David Elias, amemshukuru Katibu Mkuu kwa kutembelea maabara ya Vinasaba na kujionea namna ambavyo uchunguzi wa kimaabara unavyofanyika na pia kufahamu changamoto mbalimbali zinazowakabili watalaam wa maabara. Pia, Mkurugenzi amekiri kupokea maagizo ya Katibu Mkuu na kuhakikisha wanayafanyia kazi.



***Mkurugenzi wa Huduma za Sayansi Jinai, David Elias (wa pili kutoka kushoto), akimuonesha Dkt. John Jingu (kushoto), mazingira ya Ofisi ya Mamlaka, Dar es Salaam. Wengine kutoka kulia ni Mkurugenzi wa Huduma za Taasisi, Evaclotida Kapinga na Kaimu Mkurugenzi wa Uchunguzi wa Bidhaa na Mazingira, Dkt. Shimo Peter***



***Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Dkt. John Jingu (wa pili kutoka kushoto), akimsikiliza Meneja wa Maabara ya Sayansi Jinai Baiolojia na Vinasaba, Fidelis Bugoye (kushoto) akimuelezea namna ambavyo uchunguzi wa Vinasaba vya Binadamu unavyofanyika kupitia mitambo iliyopo katika maabara hiyo.***

# HABARI PICHA




**Picha ya kushoto:** *Mwezeshaji kutoka Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT), Pascal Duwe (aliyesimama) akiwasilisha mada mbalimbali zinazohusu usafirishaji zikiwemo Sheria, Kanuni, uendeshaji na utunzaji wa magari kwa madereva wa Mamlaka katika mafunzo ya kundi la kwanza la madereva yaliyofanyika Dodoma Oktoba 28-29, 2023.*

**Picha ya kulia:** *Watumishi wa Mamlaka kutoka Ofisi ya Kanda ya Kati, Dodoma wakifuatilia mafunzo ya huduma bora kwa mteja yaliokuwa yakitolewa na Msimamizi wa Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano kwa Umma, Sylvester Omary (hayupo pichani). Mafunzo hayo yalifanyika katika ukumbi wa Mamlaka jijini Dodoma Novemba 10, 2023.*




**Picha ya kushoto:** *Mkemia Mkuu wa Serikali, Dkt. Fidelice Mafumiko (aliyekaa katikati), akiwa pamoja watumishi kwenye hafla ya kuwapongeza watumishi wa Mamlaka kwa kufanikisha Maabara ya Chakula na Mazingira kuendelea na Ithibati baada ya kufanyiwa ukaguzi na SADCAS kwa Ithibati ya ISO17025:2017.*

**Picha ya kulia:** *Wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi wakifuatilia na kujadili taarifa mbalimbali zilizowasilishwa kwenye kikao cha Baraza la Wafanyakazi kilichofanyika Novemba 16, 2023, jijini Dar es Salaam.*




**Picha ya kushoto:** *Wanafunzi wa Udaktari wakifuatilia mafunzo yaliyokuwa yanatolewa na wataalam kutoka GCLA, kwa lengo la kuwajengea uwezo katika kufahamu majukumu ya Mamlaka ambapo wanaweza wakashirikiana katika kutekeleza majukumu yao mbalimbali ikiwemo katika ushiriki wa uchunguzi wa masuala ya jinai na kijamii ambayo yanahitaji utaalam wa madaktari na uchunguzi wa kimaabara wa Mamlaka. Mafunzo yalifanyika katika ukumbi wa chuo hicho, Novemba 30, 2023, Kilimanjaro.*

**Picha ya kulia:** *Kaimu Mkemia Mkuu wa Serikali, David Elias (aliyekaa katikati), akiwa pamoja na viongozi pamoja na wajumbe wa kikao kutoka Kurugenzi ya Huduma za Sayansi Jinai baada ya kufunga Kikao cha Menejimenti ya Mifumo ya Ubora kwa Kurugenzi ya Huduma za Sayansi Jinai kilichofanyika katika ukumbi wa Ofisi ndogo za Bunge (Austin Shaba), jijini Dar es Salaam Oktoba 30, 2023.*

# MAMLAKA YAONDOA UTATA JUU YA USAMBAZAJI WA ZEBAKI




***Meneja wa Mamlaka Ofisi ya Kanda ya Kusini, Hadija Mwema (katikati), akimsikiliza mdau aliyetembelea banda la Mamlaka kwenye Maonesho ya Fursa na Uwekezaji katika Sekta ya Madini yaliyofanyika mkoani Lindi.***

**Na Okello Thomas**

Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali imewashauri wachimbaji wa madini kuchukua tahadhari juu ya matumizi ya kemikali aina ya zebaki na *sodium cyanide* ili kujikinga na madhara ya afya pamoja na kulinda mazingira.

Mkurugenzi wa Huduma za Udhibiti kutoka Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Daniel Ndiyo aliyasema hayo wakati wa utoaji elimu kwa umma kwenye Maonesho ya Fursa na Uwekezaji katika Sekta ya Madini yaliyofanyika Ruangwa mkoani Lindi kuanzia Agosti 21 hadi 26, 2023, katika viwanja vya Ruangwa.

"Napenda nitoe wito kwa wachimbaji wadogo wanaotumia kemikali aina ya zebaki na wachimbaji wa kati wanaotumia kemikali aina ya *sodium cyanide* katika kuzalisha dhahabu kuwa, wazitumie kemikali hizi kwa kuzingatia taratibu kwa kufuata miongozo inayohitajika lakini pia kufuata taratibu ambazo zinahusisha matumizi salama yakemikali," alisema Ndiyo.

Aidha, Mkurugenzi amewasihi watumiaji wa zebaki kuendelea kutumia kemikali hiyo kwani kwa sasa inaingia nchini kwa uhalali ambapo Mamlaka imesajili baadhi ya maduka na wadau kwa ajili ya usambazaji na uuzaji kama bidhaa halali ambayo inaruhusiwa kutumika lakini kwa kuzingatia ni matumizi sahihi ikiwa ni pamoja na uvaaji wa vifaa kinga kama glovu wakati wa kukamatisha dhahabu lakini pia kujengea vyema mialo ili kuhakikisha haitasambai kwenye mazingira.

Naye, Meneja wa Mamlaka Ofisi ya Kanda ya Kusini, Hadija Mwema alisema Mamlaka itaendelea kujenga uwezo na ujuzi kwa wachimbaji kuhusu namna ya kudhibiti athari zinazotokana na utumiaji wa zebaki kwenye uchenjuaji wa dhahabu.



***Mkurugenzi wa Huduma za Udhibiti, Daniel Ndiyo (aliyevaa miwani), akiwa na Meneja wa Mamlaka Ofisi ya Kanda ya Kusini, Hadija Mwema (aliyevaa kilemba), pamoja na watumishi wa Mamlaka baada ya Maonesho ya Fursa na Uwekezaji katika Sekta ya Madini yaliyofanyika mkoani Lindi.***

# WATUMISHI WA MAMLAKA WATAKIWA KUWA WABUNIFU

**Na Okello Thomas**

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Philip Mpango amewapongeza wafanyakazi nchini kwa kuadhimisha Sikukuu ya Wafanyakazi Duniani.

Mhe. Mpango alitoa pongezi hizo wakati wa Sherehe za Maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani (Mei Mosi), yaliyofanyika kitaifa katika uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha Mei 1, 2024.

"Niwashukuru kwa mchango wenu adhimu katika ujenzi wa Taifa letu. Kama yalivyo makundi mengine kwenye jamii, kundi la wafanyakazi lina mchango mkubwa sana katika ujenzi wa nchi yetu. Serikali itaendelea kuimarisha mazingira ya kazi ikiwemo kuboresha maslahi ya wafanyakazi kadri hali ya uchumi itakavyoruhusu," alisema Dkt. Mpango.

Aidha, Makamu wa Rais alitoa wito kwa wafanyakazi, kuendelea kutekeleza majukumu yao kwa bidii, maarifa, uadilifu na kwa moyo wote, huku akiwataka kutanguliza maslahi ya Taifa mbele na kuendelea kuongeza tija katika utendaji kazi. Pia, amevisihi vyama vya wafanyakazi kushirikiana na Serikali na Waajiri kuhakikisha wanaongeza tija kwenye maeneo yao ya kazi kwa manufaa ya Taifa na wafanyakazi wenyewe, sambamba na kupaza sauti kuhusu madai ya wafanyakazi.

Kwa upande wake Meneja wa Mamlaka Ofisi ya Kanda ya Kaskazini, Eliamini Mkenga amewataka watumishi wa Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kuwa wabunifu katika utendaji kazi na pia amewashukuru watumishi wa Mamlaka kutoka kanda mbalimbali kuungana na wafanyakazi wote nchini kuadhimisha Siku ya Wafanyakazi Duniani.

Jackson Mwijage ambaye amekuwa Mtumishi Bora wa mwaka kutoka Mamlaka, amemshukuru Mkemia Mkuu wa Serikali, Dkt. Fidelice Mafumiko kwa kuwezesha watumishi kufanya kazi katika mazingira rafiki pamoja na kuwahamasisha watumishi kuendelea kufanya kazi kwa weledi ili kufikia malengo ya Mamlaka. Pia, Mwijage amewasihi watumishi kuendelea kufanya kazi kwa umoja, mshikamano, upendo na kuendelea kujituma huku wakimtanguliza Mungu.




***Watumishi wa Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali wakiwa kwenye Maandamano Siku ya Wafanyakazi Duniani (Mei Mosi), kuelekea kwenye uwanja wa Sheikh Amir Abeid - Arusha.***



***Watumishi wa Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali wakiwa kwenye Sherehe za Siku ya Wafanyakazi Duniani (Mei Mosi).***

***"Niwashukuru kwa mchango wenu adhimu katika ujenzi wa Taifa letu. Kama yalivyo makundi mengine kwenye jamii, kundi la wafanyakazi lina mchango mkubwa sana katika ujenzi wa nchi yetu. Serikali itaendelea kuimarisha mazingira ya kazi ikiwemo kuboresha maslahi ya wafanyakazi kadri hali ya uchumi itakavyoruhusu,"***
***Dkt. Mpango - Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania***

# MAMLAKA YAPONGEZWA KWA KUFANYA UCHUNGUZI KWA WAKATI

**Na Judith Lema**

Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali imepongezwa kwa kufanya uchunguzi wa kimaabara wa sampuli mbalimbali za makosa ya jinai kwa muda mfupi na kupelekea kukamilisha upelelezi kwa wakati na mashauri kusikilizwa mahakamani kwa wakati.

Pongezi hizo zilitolewa na Mkuu wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai, Mkoa wa Mtwara Mrakibu Mwandamizi wa Polisi. Adam Salim Amiri, wakati akifungua Mafunzo ya Usimamizi wa Sampuli za Makosa ya Jinai, yaliyofanyika Disemba 16, 2023, Masasi Mtwara yaliyojumuisha maafisa wa Jeshi la Polisi kutoka mikoa ya Lindi na Mtwara, Madaktari na Wataalam wa Maabara wanaohusika na mnyororo wa sampuli za makosa ya jinai.

"Napenda kuipongeza Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kwa kazi kubwa inayofanya katika uchunguzi wa kimaabara wa sampuli mbalimbali za makosa ya jinai na kusaidia kukamilisha upelelezi kwa wakati na mashauri kusikilizwa mahakamani kwa wakati na hivyo kuchangia upatikanaji wa haki kwa wakati," alisema Mrakibu Mwandamizi wa Polisi, Amiri.

Aidha, Mkuu wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai, Mkoa wa Mtwara, SSP, Amiri, alisisitiza kuwa mafunzo ya kuwajengea uwezo wadau ambao wanahusika katika mnyororo mzima wa uchukuaji wa sampuli au vielelezo na kuviwasilisha Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kwa uchunguzi wa kimaabara ni muhimu, kwa vile upatikanaji wa matokeo sahihi ya uchunguzi wa vielelezo hivyo, huchangiwa kwa kiasi kikubwa na ufanisi wa hatua za awali za uchukuaji wa vilelezo hivyo, ufungashaji na usafirishaji.

Kwa upande mwingine SSP. Amiri alidokeza umuhimu wa uchunguzi wa kisayansi katika ulimwengu wa utandawazi kuwa ndio msingi mkubwa wa kujenga kesi mahakamani.

"Niwaombe washiriki wote wa mafunzo haya kuzingatia mambo mtakayoelekezwa na kwenda kuyafanyia kazi na hatimaye kuleta mabadiliko makubwa katika kusimamia mnyororo mzima wa Haki Jinai kama anavyosisitiza Mheshimiwa Rais", alisema.

Kwa upande wake Kaimu Meneja wa Ofisi ya Kanda ya Kusini, Hosea Hosea, alisema kuwa mafunzo hayo yakitumiwa kwa usahihi yatasaidia ukusanyaji wa sampuli, ufungashaji wa sampuli na usafirishaji wa sampuli ulio sahihi ambao utasaidia Mamlaka kufanya uchunguzi na kupata majibu sahihi ambayo mwisho wa siku yatasaidia upelelezi na utoaji wa haki.

Naye, Mkuu wa Kitengo cha Jinai Mkoa wa Lindi, Mrakibu Msaidizi wa Polisi, Alton Nelson Mkonyi, akifunga mafunzo hayo alisema, mafunzo hayo yatakuwa yamefikia mafanikio iwapo washiriki wa mafunzo hayo wataenda kuyatendea kazi yale waliyojifunza na hivyo kutekeleza azma ya vyombo vya Serikali ya kutoa haki kwa watu na kwa wakati.



***Mgeni Rasmi na Mkuu wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai Mkoa wa Mtwara, Mrakibu Mwandamizi wa Polisi, Adam Salim Amiri (aliyekaa katikati) akiwa pamoja na wawezeshaji na washiriki wa mafunzo ya Usimamizi wa Sampuli za Makosa ya Jinai yaliyofanyika katika Ukumbi wa Hoteli ya Emirates Masasi Mtwara Disemba 16, 2023.***

# WATUMISHI WASHIRIKI BONANZA KUIMARISHA AFYA NA USHIRIKIANO

Na Okello Thomas

Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali imefanya bonanza la wafanyakazi wa Makao Makuu Dodoma na Ofisi ndogo ya Dar es Salaam lengo likiwa ni kuimarisha afya pamoja na kuimarisha umoja na mshikamano miongoni mwa watumishi.

Akizungumza wakati akifungua bonanza hilo lililofanyika katika fukwe za Hoteli ya South Beach Resort iliyopo Kigamboni jijini Dar es Salaam Juni 2, 2024, Mkemia Mkuu wa Serikali Dkt. Fidelice Mafumiko alisema kuwa michezo ni moja ya kipaumbele cha taasisi, hivyo ni vyema kushiriki ufanyaji wa mazoezi kwani michezo huchochea utimamu wa mwili na akili na kuboresha utendaji wa kazi.

"Afya ni mtaji, hivyo tuiunge mkono Serikali katika kuhamasisha ufanyaji wa mazoezi ili kuimarisha afya na kupambana na magonjwa yasiyoambukiza kwa hiyo, ufanyikaji wa bonanza hili sio tu kwa ajili ya afya za watumishi bali pia ni utekelezaji wa maelekezo ya Serikali. Nitoe rai kwa watumishi wenzangu kuendelea na tamaduni ya kufanya mazoezi kwasababu michezo ni afya.

Aidha, Dkt. Mafumiko amewataka watumishi kuendelea kufanya kazi kwa bidii, weledi na maarifa ili kuhakikisha taasisi inafikia malengo na kutekeleza vyema majukumu yake iliyopewa na Serikali. Pia, aliwapongeza watumishi kwa kujitokeza kushiriki katika michezo mbalimbali ikiwemo mpira wa miguu, mpira wa pete, michezo ya jadi kama vile kuvuta kamba, karata na drafti.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Huduma za Taasisi, Evaclotida Kapinga alieleza kuridhishwa na namna watumishi walivyohamasika kushiriki bonanza hilo na pia alitoa wito kwa watumishi wa Mamlaka kuendelea kujitokeza kwa wingi katika kushiriki ufanyaji wa mazoezi ya kila siku.

Naye Mwenyekiti wa Kamati ya Bonanza hilo, Ernest Lasti amemshukuru Mkemia Mkuu wa Serikali, Dkt. Fidelice Mafumiko kwa kujali suala la utimamu wa afya ya watumishi wake na ameahidi kwa niaba ya watumishi wa Mamlaka kuendelea na ufanyaji wa mazoezi kama ilivyo kwenye ratiba ya kila siku jioni baada ya kazi.



*Mkemia Mkuu wa Serikali, Dkt. Fidelice Mafumiko (katikati), akiongea wakati akifungua Bonanza kwa watumishi wa Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Makao Makuu na Ofisi ndogo lililofanyika Juni 2, 2024 katika ufukwe wa Hoteli ya South Beach Resort iliyopo Kigamboni, Dar es Salaam.*



*Watumishi wa Mamlaka (walioyaa kijani), wakishindana na timu ya Tanzanite kwenye mchezo wa mpira wa pete.*



*Mkemia Mkuu wa Serikali, Dkt. Fidelice Mafumiko (kushoto), akimkabidhi Mohammed Mdemu kombe la mshindi wa kwanza wa mpira wa miguu.*

# WENYE CHANGAMOTO YA USIKIVU WAPEWA ELIMU YA KEMIKALI

**Na Judith Lema**

Watu wenye changamoto ya usikivu (viziwi) waliopo katika Manispaa ya Mtwara, wamepatiwa mafunzo ya matumizi na utunzaji salama wa kemikali kutoka Ofisi ya Kanda ya Kusini Mtwara.

Akizungumza wakati wa ufunguzi wa mafunzo hayo yaliyofanyika Juni 13, 2024 katika Hoteli ya Laso View, Mtwara, Meneja Ofisi ya Kanda ya Kusini, Hadija Mwema, alisema kuwa mafunzo hayo yamelenga kuwapa elimu kuhusu athari za kemikali kwa vile baadhi yao wanafanya biashara ndogo ndogo zinazohusisha matumizi ya kemikali.

"Watu hawa wanafanya biashara ndogo ndogo zikiwemo utengenezaji wa batiki, utengenezaji wa sabuni na wanatumia hizi kemikali katika kufanya shughuli zao za kila siku za ujasiriamali. Hivyo kwa mafunzo haya watapata uelewa wa namna bora ya kujikinga na kutumia njia salama wakati wanatekeleza shughuli zao" alisema.

Meneja alisisitiza kuwa, kemikali ni muhimu katika kila hatua ya maisha ya mwanadamu iwe katika nyanja za kiuchumi, afya, kilimo na uzalishaji wa bidhaa mbalimbali nchini. Hata hivyo, amesema kuwa, pamoja na faida nyingi zinazoweza kupatikana kutokana na mnyororo wa biashara ya kemikali, ndani yake zinabeba hali hatarishi kwa afya na mazingira endapo zitatumika bila kufuata taratibu zilizopo.

"Wote tufahamu kuwa, kemikali zinabeba hali hatarishi ikiwemo kuwaka moto na kuleta madhara na viambata hatari kwa afya na mazingira. Ndiyo maana Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali imeandaa mafunzo haya kwa kundi hili maalumu ili kuwapa elimu ya matumizi sahihi ya kemikali na hivyo kuwawezesha kutekeleza majukumu yao ya kila siku kwa usalama zaidi huku wakilinda afya na mazingira dhidi ya athari za kemikali" alisema.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Maendeleo ya Viziwi Tanzania (TAMAVITA) Kelvin Nyema, ameishukuru Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kupitia Ofisi yake ya Kanda ya Kusini Mtwara, kwa kuwapatia elimu ya athari za kemikali kwa viziwi wa manispaa ya Mtwara. Alidokeza kuwa ni ngumu sana kwa viziwi walio pembezoni kupata mafunzo kama hayo. Hata hivyo ametoa wito kwa asasi zingine kuiga mfano wa Mamlaka ya Maabara ya Mkemia wa Serikali kwa kutoa mafunzo mbalimbali kwa viziwi kwa lengo la kuwawezesha kupata uelewa wa masuala mbalimbali.

Naye mmoja wa washiriki wa mafunzo hayo, Mwashamba Abbas, kupitia mkalimani wa lugha ya alama Ally Ewesu, ameishukuru Ofisi ya Kanda ya Kusini kuwapatia mafunzo hayo na kusema kuwa kupitia mafunzo hayo wameweza kujifunza mambo mengi sana.

"Kupitia mafunzo haya tumeweza kujifunza kuhusu matumizi salama ya kemikali na madhara ambayo yanaweza kutokea kutokana na matumizi mabaya ya kemikali na pia tumeweza kujifunza namna ya kujikinga na madhara ya kemikali, mambo ambayo viziwi kuyafahamu ilikuwa ni ngumu sana". Alisema Mwashamba.



***Meneja, Ofisi ya Kanda ya Kusini, Hadija Mwema, (katikati waliokaa) akiwa na washiriki wa Mafunzo ya Matumizi na Utunzaji Salama wa Kemikali kwa watu wenye changamoto ya usikivu (viziwi) kutoka Manispaa ya Mtwara, mara baada ya kukamilika kwa mafunzo hayo, wengine katika picha ni Mtendaji Mkuu, Taasisi ya Maendeleo kwa Viziwi Tanzania (TAMAVITA) Makao Makuu Dodoma, Kelvin Nyema (kulia waliokaa), Mtumishi wa Mamlaka kutoka Ofisi ya Kanda ya Kusini Mtwara, Hosea Hosea (kushoto waliokaa) na Mtumishi wa Mamlaka kutoka Kanda ya Kusini Mtwara, Elisha Kibonde (wa kwanza kulia waliosimama).***



***Lightness Msuya (aliyesimama) akiuliza swali kuhusu Utaratibu wa kupata vipimo vya kujua uhalali wa mtoto kwa mzazi Mafunzo ya Matumizi na Utunzaji Salama wa Kemikali kwa watu wenye changamoto ya usikivu (viziwi) kutoka Manispaa ya Mtwara.***

# WANAFUNZI WATAKIWA KUTUMIA FURSA KWENYE ELIMU



***Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Dkt. John Jingu (kulia), akimkabidhi cheti Malaika Wankanga ambaye alikuwa mshindi wa kwanza kitaifa kwa upande wa wasichana katika somo la kemia mwaka 2022.***

**Na Judith Lema**

Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA) imetoa zawadi kwa wanafunzi na walimu waliofanya vizuri zaidi kitaifa kwenye masomo ya Kemia, Fizikia na Baiolojia kidato cha Nne, 2022 na Kidato cha sita 2023.

Akizungumza wakati wa kutoa zawadi hizo Juni 7, 2024 jijini Dar es Salaam, Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Dkt. John Jingu alisema kuwa wanafunzi hao wanastahili pongezi kwa kufanya vizuri zaidi kitaifa katika masomo ya sayansi na kutumia vizuri fursa ambayo Serikali imewekeza katika sekta ya elimu nchini.

"Wanafunzi mmefanya vizuri katika masomo yenu na ndiyo maana leo hii tupo hapa kwa lengo moja tu la kuwapongeza kwa sababu mmefanya jambo kubwa, jambo zuri. Mnastahili pongezi, huu uwekezaji ambao Rais Samia anaendelea kufanya kwenye sekta zote, sasa nyie mmetumia fursa hiyo vizuri na leo tunawapongeza" alisema.

Dkt. Jingu, alisema kuwa Sayansi ni dunia ya leo na ya kesho na ndiyo inayotoa majawabu ya mambo makubwa ya mustakabali wa maisha yetu, iwe kwenye kilimo, ufugaji, afya na mengineyo. Amesema kuwa Serikali imeendelea kuwekeza katika maeneo ya sayansi, uwekezaji mkubwa kuanzia shuleni hadi kwenye vyuo vya mafunzo ili wanafunzi waive vizuri na kuwa mahiri na kuleta majawabu ya changamoto mbalimbali zinazoikabili jamii.

Akizungumza kuhusu Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali Dkt. Jingu alisema GCLA ni chombo muhimu sana katika Maisha ya nchi yetu na pia kwenye sekta ya afya ni moja ya nguzo kubwa na kwenye mnyororo wa haki jinai husaidia vyombo vinavyohusika na utoaji wa haki jinai, kutenda kazi zao vizuri katika kuleta haki na kwa jamii husaidia kupata majawabu ya kisayansi.

"Natoa wito kwa Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kuendeleza zoezi hilo na kuongeza ubunifu wa mara kwa mara wa kuwazawadia wanaofanya vizuri na kuendelea kushirikiana na watoa mafunzo ili mwisho wa siku jamii iweze kuchangia kupata wanasayansi walioandaliwa vizuri na wenye kutoa majawabu" alisema Katibu Mkuu.

Vile vile alitoa wito kwa wadau wengine kuongeza nguvu na uwekezaji kwenye maeneo ya sayansi ili wanasayansi wetu wapate mazingira mazuri ya kusoma.

"Ni muhimu sana tuendelee kuwekeza katika eneo la sayansi, tuwe na wanasayansi mahiri ambao watajibu masuala makubwa ambayo yanayosumbua maisha yetu katika nyanja mbalimbali, kwani dunia ya leo na dunia ya kesho itatanabainishwa na sayansi, kwa hiyo lazima tuendelee kuwekeza katika maeneo ya sayansi," aliongeza Dkt. Jingu.

Aidha, aliwashukuru wazazi na walezi kwa malezi mazuri kwa vijana hao na kueleza kuwa malezi ndiyo yanaamua mustakabali wa mtoto achukue mkondo upi wa maisha. Amesisitiza kuwa wazazi ndio wanaotengeneza dunia na ikiwa wazazi wataacha kutimiza wajibu wao kama walezi matokeo yake ni kupata watu katika jamii wanaokuwa mzigo, amewasisitiza wazazi kuwekeza kwenye maadili mazuri kwa watoto wao ikiwa ni pamoja na kupenda kufanya kazi na kuwa na tabia njema.

Kwa upande wake Mkemia Mkuu wa Serikali, Dkt. Fidelice Mafumiko, amesema, jumla ya wanafunzi 384 wametunukiwa vyeti tangu kuanzishwa kwa utaratibu huo mwaka 2007 na walimu 48 wamepongezwa. Amesema, Mamlaka ina mpango wa kuongeza kuwatunuku wanafunzi watakofanya vizuri zaidi kitafa katika somo la Hisabati kuanzia 2025.

Naye Munge Daniel, mwakilishi wa Wanafunzi waliofanya vizuri kitaifa katika masomo ya Sayansi akiongea kwa niaba ya wanafunzi wenzake amesema kuwa pongezi na zawadi hizo zimewapa motisha kubwa sana kwao kwa vile zinawapa hamasa kuendelea kupigania ndoto zao ziweze kuishi, na pia zinawapa hamasa wadogo zao na wanafunzi wengine kufanya bidii ili nao wafikie hatua kama yao.

Mwakilishi wa Wazazi ambaye pia ni Katibu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Nenelwa Mwihambi, akiongea kwa niaba ya wazazi wa watoto waliofanya vizuri zaidi kitaifa kwenye masomo ya sayansi ameishukuru Serikali kupitia Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kwa wazo hilo zuri na ubunifu huo ambao amesema unaleta motisha kubwa sana kwa Watoto na kwa wazazi pia. Aidha, amewashukuru wanafunzi hao kwa kuwaheshimisha na pia amewashukuru walimu kwa kuwawezesha wanafunzi hao kufikia hatua hiyo.

# WAKAGUZI WATAKIWA KUONGEZA UFANISI

**Na Sylvester Omary**

Mkemia Mkuu wa Serikali, Dkt. Fidelice Mafumiko, amewataka Wakaguzi wa Kemikali na Maabara za Kemia kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yao kwa lengo la kuleta tija na kuongeza mapato kwa Mamlaka.

Mkemia Mkuu wa Serikali, aliyasema hayo Juni 9, 2024 wakati akifunga kikao kazi cha mwaka cha Wakaguzi wa Kemikali na Maabara ya Kemia kilichofanyika katika Ofisi za Makao Makuu ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali jijini Dodoma.

"Tunapaswa kuzidisha juhudi ya kuongeza vyanzo vya mapato ili kuweza kuleta ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yetu. Tunapaswa kutambua huu ni wajibu wetu na tusipotekeleza sisi hakuna atakayeweza kutekeleza. Maazimio yote tuliyokubaliana katika kikao hiki tukayafanyie kazi na kuyawekea mkakati wa kuyatekeleza na nani anatekeleza ili isije kuwa na mshangao tutakapokuja kukutana tena kwenye kikao kijacho.

Tutaangalia namna bajeti itakavyokuwa ili ikiwezekana vikao hivi kufanyika mara mbili kwa mwaka badala ya mara moja. Naamini kamati kwa kushirikiana na wataalam wa fedha tunaweza kufanikisha hili katika mwaka wa fedha 2024/2025 ingawa bajeti imeshapitishwa, kupanga ni kuchagua naamini inawezekana" alisema Dkt. Mafumiko.

Aidha, amezipongeza ofisi za Kanda kwa kujitahidi kukusanya mapato hali iliyopelekea kuwa zaidi ya asilimia sabini kwa baadhi ya Kanda huku Kanda ya Mashariki ikiwa kwenye asilimia tisini na moja, hali iliyopelekea kuanza kutoa tuzo kwa baadhi ya Wakaguzi waliofanya vizuri zaidi kwenye maeneo yao ya kazi.

"Mawasilisho yaliyowasilishwa na Meneja wa Kanda yameonesha kuleta mafanikio katika ukusanyaji wa mapato kwa sababu hakuna sehemu ambayo tuko chini ya asilimia 70. Hatua hii tuliyofikia tunapaswa kujipongeza kwa sababu wote tumechangia na tunapaswa kuendelea kuongeza nguvu zaidi ili kufikia malengo tunayojiwekea. Kupitia mkutano huu tutatoa zawadi kwa wakaguzi na waratibu wa ukaguzi na usajili wa kanda na wa Makao Makuu. Kwa kuanza tutaanza na hizi mbili na Utaratibu huu utakuwa unafanyika kila mwaka ikiwa ni sehemu ya kuwapa motisha ya utendaji kazi kwa wakaguzi wa Mamlaka. Katika mwaka ujao tutaanza kutoa zawadi hizi kwa Ofisi za Kanda ambazo zimefanya vizuri zaidi katika utekelezaji wa majukumu yake" alimaliza Mkemia Mkuu wa Serikali.

Akiongea baada ya kupokea tuzo ya Mkaguzi bora zaidi kutoka Ofisi ya Kanda ya Kati, Revocatus Mwamba, ameshukuru kwa kupokea tuzo hiyo na anaamini itamfanya kuongeza juhudi zaidi katika utekelezaji wa majukumu.

"Kwanza namshukuru sana Mkemia Mkuu wa Serikali kwa kuweza kutoa tuzo hizi, binafsi sikutarajia kama kuna kitu kama hiki kwa sababu huwa natekeleza majukumu yangu kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu kama mtumishi wa Umma. Kumbe tunapofanya hivyo kuna watu wengine wanatuangalia na kuona kile tunachokifanya kwa namna nyingine inatia moyo sana. Tuzo hii kwangu imeongeza hali zaidi katika kutekeleza wa majukumu yangu na inanifanya kujituma katika kazi na nawasihi watumishi wenzagu kutambua kwamba tunapotekeleza kazi zetu kuna watu wanatuangalia na kutupima" alisema Mwamba.



***Mkemia Mkuu wa Serikali, Dkt. Fidelice Mafumiko (kulia), akimkabidhi tuzo Georgina Kilindo (kushoto), kwa kufanya vizuri katika ukaguzi wa kemikali na usajili wa kemikali katika Mkutano Mkuu wa mwaka wa Wakaguzi wa Kemikali na Maabara za Kemia uliofanyika kwa siku mbili kuanzia Juni 8 hadi 9, 2024, jijini Dodoma.***



***Mkemia Mkuu wa Serikali, Dkt. Fidelice Mafumiko (katikati), akiwa na viongozi pamoja na washiriki wa Mkutano Mkuu wa mwaka wa Wakaguzi wa Kemikali na Maabara za Kemia uliofanyika kwa siku mbili kuanzia Juni 8 hadi 9, 2024, jijini Dodoma.***

# WADAU WATAKIWA KUWA NA UELEWA WA KEMIKALI

**Na Mwanaheri Jazza**

Taasisi za Umma na binafsi zimetakiwa kutenga bajeti Kwa ajili ya kuwawezesha wataalam wanaojishughulisha na masuala ya kemikali kuendelea kupata elimu sahihi ya matumizi salama ya kemikali ili kulinda Afya zao pamoja na mazingira.

Akizungumza mkoani Kigoma katika mafunzo ya kuwajengea uelewa wa Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Kemikali kwa taasisi za umma na wadau wa kemikali, Mkurugenzi wa huduma za Udhibiti kutoka Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Daniel Ndiyo, alisema wataalam hao wanapokuwa na elimu sahihi kuhusu kemikali watailinda jamii yote na watanzania kwa ujumla na kuwa nafasi kubwa ya kufanya kazi.

"Niziombe Taasisi za Umma, binafsi pamoja na waajiri wengine wote ambao wanajihusisha na masuala ya kemikali wajitahidi kutenga bajeti Kwa ajili ya kuwawezesha wataalam wa kemikali kupata elimu sahihi Kwa sababu mtu anapokuwa na elimu sahihi kuhusiana na matumizi ya kemikali atamlinda mwenzake, atailinda jamii ya Watanzania, vile vile atajilinda yeye mwenyewe anapotekeleza majukumu yake," alisema Daniel Ndiyo.

Akimwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Kigoma, Thobias Andengenye, katika mafunzo hayo, Katibu Tawala Msaidizi wa Biashara na Uwekezaji Kigoma, Deogratius Sangu, amewataka wadau hao kusimamia Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Kemikali za Viwandani na Majumbani Namba 3 ya Mwaka 2003, pamoja na Kanuni zake za Mwaka 2020, pindi wanapotekeleza majukumu yao.

"Ndugu washiriki Mkoa wa Kigoma ukiwa ni sehemu ya nchi hii na ukiwa na bandari za kuingiza au kutoa shehena za kemikali nchini, nao pia unaguswa na matakwa ya Sheria hii"alisema," Deogratius Sangu.

Kwa upande wake mshiriki wa mafunzo hayo kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Gwakisa Maseba, alisema mafunzo hayo yameongeza uwezo na ari ya kufanya kazi kwa bidii pamoja na kuimarisha ushirikiano na wataalamu wa kemikali.

"Kwetu sisi mafunzo haya yametuongezea uwezo na ari ya kufanya kazi, lakini pia kuona jinsi ambavyo tutaweza tukashirikiana na wataalamu wa kemikali na hata wataalamu kutoka idara nyingine katika maeneo yetu ya kazi ili kuona kwamba tunafanya hivyo katika kutekeleza wajibu wetu na pia kuzingatia Sheria na taratibu zote zinazohusiana na kemikali zinafuatwa," alisema Gwakisa.



***Meneja wa Mamlaka Ofisi ya Kanda ya Ziwa, John Wanjala akielezea utekelezaji wa Sheria ya Kemikali pamoja na Sheria zingine kwenye Mafunzo kwa Maafisa wa Serikali juu ya Usimamizi wa Kemikali yaliyofanyika katika ukumbi wa Bandari – Kigoma Juni 11, 2024.***



***Washiriki wa Mafunzo wakifuatilia mada mbalimbali kwenye mafunzo ya matumizi salama ya kemikali kwa wadau yaliyofanyika Juni 12, 2024.***



***Mshiriki wa mafunzo ya matumizi salama ya kemikali, akichangia mada zilizowasilishwa na wataalam kutoka Mamlaka.***

# GCLA YAAGIZWA KUSAIDIA WAATHIRIKA WA KEMIKALI

**Na Mwanaheri Jazza**

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mh. Dkt Philip Mpango ameitaka Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kushirikiana na wizara ya Afya kufika katika hospitali ya Kibong'oto iliyopo wilayani Moshi Mkoa wa Kilimanjaro ili kuwasaidia vijana walioathirika na kemikali.

Makamu wa Rais, Dkt Mpango aliyasema hayo Juni 20, 2024 jijini Dodoma wakati alipotembelea Banda la Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali katika ufunguzi wa maonesho ya Wiki ya Madini yanayofanyika katika ukumbi wa Jakaya Kikwete.

"Vijana wengi hasa wanaofanya kazi kwenye madini wameathirika na kemikali na hivyo wanahitaji kusaidiwa. Sasa niwape jukumu, fanyeni utaratibu wa kuzungumza na wizara ya Afya mkatembelee hospitali ya Kibong'oto muone jinsi ambavyo vijana wetu wanaofanya kazi huko hasa kwenye madini walivyoathirika sana na mojawapo ya hizo kemikali. Nataka muende ili muone uzito wa tatizo ili muongeze nguvu ya kuwasaidia" alisema Dkt Mpango.

Kwa upande wake Meneja wa Ofisi ya Kanda ya Kati wa Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Gerald Meliyo ameahidi kutekeleza maelekezo hayo yaliyotolewa na Makamu wa Rais, Dkt Philip Mpango.

"Sisi kama Mamlaka tunaahidi kutekeleza maagizo aliyoyatoa Makamu wa Rais, Dkt Mpango ya kutembelea katika hospitali ya Kibong'oto kuona hali halisi ya wagonjwa, lakini pia kuwa na mkakati maalum wa kupunguza madhara ya kemikali kwa wachimbaji wadogo wa dhahabu na madini mengine na pia tutahakikisha kwamba tunawafikia na kutoa elimu hasa ya matumizi sahihi ya kemikali" alisema Meliyo.

Awali akifungua maonesho hayo Makamu wa Rais Dkt Mpango amewataka wachimbaji wa madini kuacha uharibifu wa mazingira unaosababishwa na shughuli za uchimbaji mdogo wa madini na kupelekea kuwepo kwa mashimo yaliyotelekezwa baada ya uchimbaji wa madini, ikiwa ni pamoja na ukataji wa misitu kwa ajili ya kupanua maeneo ya uchimbaji, uharibifu wa vyanzo vya maji na matumizi holela ya kemikali ya zebaki.

"Naomba nitumie fursa hii kuwaasa kuwa na uchimbaji endelevu ambao unazingatia urejeshaji wa ardhi kwa baadhi ya uchimbaji ili kulinda hifadhi ya mazingira ikiwemo uoto wa asili, vyanzo vya maji na kurejesha maeneo yaliyotumika kwa uchimbaji katika hali yake ya asili ili yaweze kutumika kwa shughuli zingine za kiuchumi" alisema Makamu wa Rais.

Maonesho ya wiki ya madini yamefunguliwa rasmi Juni 20, 2024 ambapo yamebeba kauli mbiu isemayo "Amani iliyopo Tanzania ilete soko la madini Afrika nchini Uchumi Imara" na yanatarajiwa kuhitimishwa Juni 27, 2024.



***Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Philip Mpango (kulia) akitoa maelekezo kwa Meneja wa Ofisi ya Kanda ya Kati, Gerald Meliyo (kushoto) baada ya Makamu wa Rais, kutembelea banda la Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kwenye maonesho ya Wiki ya Madini yaliyofanyika katika ukumbi wa Jakaya Kikwete jijini Dodoma, Juni 20, 2024.***

*"Vijana wengi hasa wanaofanya kazi kwenye madini wameathirika na kemikali na hivyo wanahitaji kusaidiwa. Sasa niwape jukumu, fanyeni utaratibu wa kuzungumza na wizara ya Afya mkatembelee hospitali ya Kibong'oto muone jinsi ambavyo vijana wetu wanaofanya kazi huko hasa kwenye madini walivyoathirika sana na mojawapo ya hizo kemikali. Nataka muende ili muone uzito wa tatizo ili muongeze nguvu ya kuwasaidia"*

*Dkt Philip Mpango*
*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania*

## HABARI PICHA





**Picha ya kushoto:** *Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Aretas Lyimo (kushoto), na mwenyeji wake Mkemia Mkuu wa Serikali, Dkt. Fidelice Mafumiko, wakimsikiliza Mtumishi wa Mamlaka, Msafiri Mwasyeba (kulia), akielezea namna mtambo wa LCMS unavyofanya uchunguzi wa dawa za kulevya.* **Picha ya kulia:** *Mtumishi wa Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Hussein Yassini (wa pili kutoka kushoto) akitoa maelezo ya namna ya kutumia mtambo wa FT-IR kwa watumishi wa Chuo cha Nelson Mandela cha jijini Arusha walipotembelea maabara ya mitambo.*






**Picha ya kushoto:** *Mkemia Mkuu wa Serikali, Dkt. Fidelice Mafumiko (kati kati waliokaa), akiwa na watumishi ma Mamlaka walioshiriki mazoezi ya pamoja Mei 4, 2024.* **Picha ya kulia:** *Mkurugenzi wa Huduma za Sayansi Jinai, David Elias (aliyevaa tai), akiwa pamoja na wataalam wa maabara kutoka GCLA pamoja na wakufunzi kutoka Finland baada ya mafunzo yaliyofanyika katika ukumbi wa Ofisi ndogo ya Mamlaka Dar es Salaam Mei 20, 2024.*






**Picha ya kushoto:** *Kaimu Meneja wa Maabara ya Chakula na Dawa, Everlight Matinga (kulia) akizungumza na mwanafunzi wa Shule ya Sekondari Elboru iliyopo jijini Arusha Aprili 17, 2024.* **Picha ya kulia:** *Mtaalam wa Maabara kutoka GCLA, Ernest Lasti (kati kati), akiwaonesha wakufunzi kutoka Finland mitambo mbalimbali ya uchunguzi.*

# SHULE YA SEKONDARI GOGONI YAPEWA VIFAA VYA MAABARA




***Meneja wa Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Kanda ya Mashariki, Danstan Mkapa (kushoto), akikabidhi vifaa vya maabara kwa viongozi wa shule ya Sekondari ya Gogoni iliyopo Kibamba jijini Dar es Salaam Oktoba 14, 2023.***

Na Jackson Monela

Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali imetoa msaada wa vifaa vya maabara vyenye thamani ya zaidi ya Shilingi Milioni 4 kwa shule ya Sekondari ya Gogoni iliyopo Kibamba jijini Dar es Salaam.

Akikabidhi vifaa hivyo Oktoba 14, 2023, katika Mahafali ya kumi na moja ya shule hiyo kwa niaba ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Meneja wa Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Kanda ya Mashariki, Danstan Mkapa, alisema Mamlaka hiyo imeamua kutoa vifaa hivyo ili kuwatia motisha wanafunzi wanaosoma masomo ya sayansi, kuweza kufanya vizuri kwenye masomo hayo.

"Naomba niwakabidhi vifaa hivi kutoka kwa Mkemia Mkuu wa Serikali, ikiwa ni mchango wake kwa shule hii ikiwemo kuhakikisha wanafunzi wanaosoma masomo ya Sanyansi wanapata nafasi ya mafunzo kwa vitendo kwa ufanisi."alisema Mkapa.

Akipokea vifaa hivyo, Mwalimu Mkuu wa Shule hiyo, Charles Komba, ameishukuru Mamlaka hiyo kwa kuwapatia msaada huo, ambapo amesema vitawasaidia wanafunzi wanaochukua masomo ya Sayansi kuweza kufanya mafunzo kwa vitendo vizuri tofauti na hapo awali walikuwa wakishindwa kufanya kutokana na changamoto upungufu wa vifaa iliyokuwa ikawabili.

Katika Hatua nyingine Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali imetumia mahafali hayo kama jukwaa la kutoa elimu ya Matumizi salama ya kemikali ambapo wananchi waliohudhuria sherehe hiyo wameweza kupatiwa elimu hiyo ikiwemo elimu ya athari za kemikali endapo hazitotumiwa kwa uangalifu.



***Meneja wa Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Kanda ya Mashariki, Danstan Mkapa (aliyevaa skafu), akishuhudia wanafunzi wa shule ya Sekondari ya Gogoni iliyopo Kibamba jijini Dar es Salaam wakifanya majaribio ya kisayansi (experiments/practice).***

## HABARI PICHA




***Meneja wa Ofisi ya Kanda ya Mashariki Danstan Mkapa (kulia), akimkabidhi cheti cha usafirishaji salama wa kemikali mshiriki wa mafunzo hayo yaliyofanyika katika ukumbi wa Dar es Salaam Corridor Group (DCG), Machi 22, 2024. Mafunzo hayo yalitolewa kwa zaidi ya madereva 45 kutoka kampuni ya DCG.***



***Mkemia Mkuu wa Serikali Dkt. Fidelice Mafumiko (katikati), akizungumza na wafanyakazi wa mgodi wa Geita Gold Mining alipotembelea kampuni hiyo pamoja na Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka Profesa Esther Lugwisha ((wa tano kutoka kushoto), wakati wa ziara ya kikazi Kanda ya Ziwa Machi 5, 2024.***

## HABARI PICHA



***Meneja wa Ofisi ya Kanda ya Kusini – Mtwara, Hadija Mwema (aliyesimama), akifafanua jambo kuhusu Sheria ya Udhibiti na Usimamizi wa Kemikali katika mafunzo ya usafirishaji salama wa Kemikali kwa madereva yaliyofanyika mjini Songea mkoani Ruvuma Machi 14, 2024. Katikati ni Mkurugenzi wa Huduma za Udhibiti, Daniel Ndiyo.***



***Wananchi wakishuhudia zoezi la uondoaji wa kemikali iliyomwagika barabarani katika eneo la ajali ya kemikali iliyotokea Mbala Kijiweni mkoani Pwani Februari 18, 2024, ili kulinda afya ya wananchi na mazingira pamoja na kuruhusu magari ya pande zote mbili kuendelea na safari.***

## HABARI PICHA




***Mkemia Mkuu wa Serikali Dkt. Fidelice Mafumiko (kushoto), akimkabidhi tuzo Mwanamke aliyefanya vizuri zaidi katika Sekta ya Mavazi 'Best Textile Fashion Design Company of the Year' katika Sherehe za Msimu wa Nne wa Utoaji Tuzo za Viwanda kwa Wanawake Wajasiriamali 2024, katika ukumbi wa The Super Dome Dar es Salaam Machi 12, 2024.***



***Wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi la Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali wakifuatilia taarifa kuhusu utekelezaji wa shughuli mbalimbali za uendelezaji wa Mamlaka kutoka kwa wawasilishaji mbalimbali (hawapo pichani), Kikao cha Tano cha Baraza la Saba la Wafanyakazi wa Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA), kilichofanyika katika Ukumbi wa PSSSF Commercial Complex, jijini Dar es Salaam, Februari 15, 2024.***

## HABARI PICHA



**_Mkemia Mkuu wa Serikali, Dkt. Fidelice Mafumiko (aliyesimama), akizungumza wakati wa kikao na wadau wa Mamlaka kutoka Kanda ya Mashariki kilichofanyika katika ukumbi wa Mamlaka jijini Dar es Salaam Juni 20, 2024 ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Maadhmisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma ambapo Mtendaji Mkuu anahitajika kukutana na Wadau wa ndani na nje na kuwasikiliza kuhusiana na masuala ya utoaji huduma na changamoto nyingine kwa ajili ya kuzipokea na kuzitafutia ufumbuzi._**

**_Wa pili kutoka kushoto ni Meneja wa Mamlaka Ofisi ya Kanda ya Mashariki, Danstan Mkapa pamoja na washiriki wengine wa kikao hicho kutoka Mamlaka._**



**_Viongozi waliotembelea mradi wa ujenzi wa nyumba ya watumishi katika mpaka wa Kabanga, wakipata maelezo kutoka kwa mmoja wa mafundi wa nyumba hiyo._**

# MASWALI YAULIZWAYO MARA KWA MARA

## NI NANI WANAWEZA KULETA SAMPULI KWA AJILI YA UCHUNGUZI?

Sampuli kwa ajili ya uchunguzi huweza kuletwa na wamiliki wa viwanda, wajasiriamali wakubwa na wadogo, mtu binafsi,Taaisisi za Serikali, mashirika binafsi na asasi zisizo za kiserikali.

## TOFAUTI KATI YA MAMLAKA YA DAWA NA VIFAA TIBA (TMDA),SHIRIKA LA VIWANGO TANZANIA (TBS) NA MAMLAKA YA MAABARA YA MKEMIA MKUU WA SERIKALI (GCLA)

- Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) ina wajibu wa kulinda afya ya jamii kwa kuhakikisha ubora na usalama wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi.
- Shirika la Viwango Tanzania (TBS) majukumu yake ni kusimamia na kulinda ubora wa bidhaa na chakula katika sekta ya viwanda na biashara.
- Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA) kisheria ndiyo Maabara Kuu ya Rufaa ya Serikali kwenye masuala yote yanayohusu uchunguzi wa kimaabara na matokeo yake ni ya mwisho. Maabara pekee ya Serikali yenye jukumu la kufanya uchunguzi wa vielelezo vyote ikiwemo vielelezo vya vyakula na dawa pale vinapohusisha jinai au pale sampuli/vielelezo hivyo vinapohusisha maslahi ya taifa.

## NI SAMPULI GANI ZINAWEZA KUFANYIWA UCHUNGUZI KWENYE KURUGENZI YA UCHUNGUZI WA BIDHAA NA MAZINGIRA?

Ni sampuli za vyakula, dawa na malighafi za dawa, dawa asili, viungo vya chakula, vipodozi, maji taka, udongo, detergents, sediments,kemikali na mazao yake.

## GHARAMA YA UCHUNGUZI VINASABA ZIKOJE?

Ghrama za uchunguzi ni shilingi 100,000/= kwa sampuli moja yaani mtu mmoja. Hivyo kwa wahusika watatu (yaani baba, mama na mtoto) ni shilingi laki tatu 300,000/=

## MAHITAJI YA KIPIMO CHA VINASABA KABLA YA KUCHUKULIWA KIPIMO CHA VINASABA YAKOJE?

Mwombaji anapaswa apate barua ya maombi kutoka Mamlaka zinazotambulika kisheria ambazo ni:

- Mahakama kwenye masuala ya jinai na kijamii
- Mawakili waliosajiliwa na wanatambulika kisheria
- Ustawi wa jamii
- Polisi mwenye cheo cha kuanzia mkaguzi
- Mkuu wa Wilaya kwenye majanga ya kitaifa
- Madaktari kwenye masuala ya tiba
- Taasisi au vituo vya utafiti vilivyosajiliwa

## KITUO CHA KUDHIBITI MATUKIO YA SUMU NCHINI NI NINI ?

Ni kituo cha kudhibiti matukio ya sumu nchini, kilichopo chini ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, kinachofanya kazi ya kudhibiti matukio ya sumu nchini kwa kushirikiana na taasisi za tiba ili kusaidia watu wanaoathirika na sumu.



# Wasiliana nasi

## Anwani/Mahali

MAMLAKA YA MAABARA YA MKEMIA MKUU WA SERIKALI
5 BARABARA YA MKEMIA MKUU WA SERIKALI
MTAA WA SECHERELA,
KATA YA TAMBUKARELI,
KITALU Na 138 & 140,
KIWANJA 'AC'
S.L.P 2925, 41104 DODOMA

Tupigie
Simu: (+255)0262161630

Barua pepe
gcla@gcla.go.tz

Nukushi
+255 27 2506394

## Anwani/Mahali

Meneja
Ofisi ya Kanda ya Kaskazini
Kitalu Na 3, Sekei
S.L.P 2095,
Arusha,Tanzania

Tupigie
Simu: +255 27 2506394

Barua pepe
gcla.north@gcla.go.tz

Nukushi
Email: gcla.north@gcla.go.tz

## Anwani/Mahali

Meneja
Ofisi ya Kanda ya Nyanda za Juu kusini
Kitalu F Iwambi.
S.L.P 2875
Mbeya. Tanzania.

Tupigie
Simu: +255 25 2502311

Barua pepe
gcla.southern@gcla.go.tz

Nukushi
+255 25 2502312

## Anwani/Mahali

Meneja
Ofisi Ya Kanda ya Mashariki
Mtaa wa Luthuli
S.L.P 164 164
Dar Es Salaam-Tanzania.

Tupigie
Piga Bure: +255 22 2113320
Simu: +255 (0)737 878020

Barua pepe
gcla.east@gcla.go.tz

Nukushi
+255 22 2113320

## Anwani/Mahali

Meneja
Ofisi ya Kanda ya Ziwa
Hospitali ya Sekou Toure / Eneo la Isamilo,
S.L.P 502,
Mwanza-Tanzania

Tupigie
Simu: +255 28 2500279

Barua pepe
gcla.lake@gcla.go.tz

Nukushi
+255 28 2500279

## Anwani/Mahali

Meneja
Ofisi Kanda ya Kusini,
Barabara ya Mahakama
S.L.P 1414
Mtwara,Tanzania

Tupigie
Simu: +255 23 233 4760

Barua pepe
gcla.south@gcla.go.tz

Nukushi
+255 23 233 4761



**HATARI SUMU**

**Piga simu kituo cha kudhiti matukio ya sumu unapokuwa na wasiwasi ya tukio la sumu kwa simu ya BURE 0800112031 au 022 2221410 kwa msaada na ushauri.**